PANDA MITI KIBIASHARA

PARTICIPATORY PLANTATION FORESTRY PROGRAMME

# PARTICIPATORY PLANTATION FORESTRY PROGRAMME

## MWONGOZO WA UWEZESHAJI WA UANZISHWAJI NA UIMARISHWAJI WA VIKUNDI VYA WAKULIMA WA MITI

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

Embassy of Finland
Dar es Salaam

# MWONGOZO WA UWEZESHAJI WA UANZISHWAJI NA UIMARISHWAJI WA VIKUNDI VYA WAKULIMA WA MITI

**Disemba 2020, Iringa, Tanzania**



© INDUFOR: TGA Guideline.Pdf

# Mwongozo Wa Uwezeshaji Wa Uanzishwaji Na Uimarishwaji Wa Vikundi Vya Wakulima Wa Miti

## Participatory Plantation Forestry Programme – PFP-2 (Pandamiti Kibiashara)

**Waandishi wa ripoti:**

| | |
|---|---|
| Thomas Selänniemi | Mshauri |

**Wachangiaji wengine:**

| | |
|---|---|
| Kastory Timbula | Meneja, TTGAU |
| Simon Kiteeja | Mwalimu, FTI |
| Raheli Swai | Meneja, FWITC |
| Chamba Pamba | Mkufunzi, FWITC |
| Joyce Msigwa | Mtaalamu wa uchumi jamii, PFP-2 |

**Panda Miti Kibiashara**
Kiwanja na.21, Kitalu 1, Kanda 1A
Gangilonga
S.L.P 2244, Iringa.

www.privateforestry.or.tz

## YALIYOMO

1. UTANGULIZI ........ 5
1.1 Muhtasari ........ 5
1.2 Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU) ........ 5
2. KANUNI ZA MSINGI KATIKA UWEZESHAJI WA UANZISHWAJI NA UIMARISHARIJI WA TGA ........ 7
2.1 "Utayari wa kutaka kuwa na ushirikiano" ndiyo msingi wa kuanzishwa kwa TGA........ 7
2.2 Sehemu ya kuanzia katika kijiji ni kwenye TGA iliyopo au vikundi vya wakulima wa miti........ 7
2.3 Kuimarisha TGA ni kuhusu kikundi........ 8
2.4 Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu(HRBA) na ujumuishishwaji inatoa mfumo ........ 8
2.5 Viashiria vinatoa uelekeo kwa ajili ya uimarishaji wa TGA........ 8
2.6 Mchakato ulioundwa vizuri na endelevu kwa ajili ya uwezeshaji wa TGA ........ 9
2.7 Uhalisia wa TGA utawale usaidizi na ujuzi unaojitosheleza baina ya wawezeshaji ni msingi ........ 9
2.8 Ushirikiano na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU) na watoa huduma wengine ili kukuza uendelevu ........ 10
3. VIASHIRIA - SIFA ZA TGA IMARA ........ 11
3.1 Utawala na Usimamizi ........ 11
3.1.1 Usajili na nyaraka za uanzilishaji ........ 11
3.1.2 Uongozi, mikutano na ofisi ........ 11
3.1.3 Fedha na usimamizi wa mali ........ 12
3.1.4 Mipango na taratibu za kupanga mipango ........ 12
3.1.5 Ushirikishanaji taarifa ........ 13
3.2 Utoaji huduma kwa wanachama........ 13
3.2.1 Utoaji huduma na utaratibu wa kutoa mrejesho........ 13
3.3 Hatua muhimu - Taarifa kuongoza ukuaji wa TGA kufikia viashiria ........ 13
4. KUWEZESHA UANZISHWAJI WA KIKUNDI CHA WAKULIMA WA MITI........ 15
4.1 Utangulizi ........ 15
4.2 Hatua ya 1: Uhamasishaji........ 15
4.2.1 Mikutano ya maandalizi kabla ya kujihusisha katika kijiji ........ 15
4.2.2 Mikutano katika ngazi ya kijiji ........ 16
4.3 Hatua ya 2: Uanzishwaji ........ 17
5. UIMARISHAJI KIKUNDI CHA WAKULIMA WA MITI ........ 20
5.1 Mfumo ........ 20
5.2 Kujenga uwezo wa TGA juu ya utawala na usimamizi ........ 20
5.2.1 Mafunzo mahusi kwa uongozi wa TGA........ 21
5.2.2 Kuwawezesha wanachama wa TGA........ 22
5.2.3 Mipango na Upangaji - kuimarisha viongozi na mitazamo ya wanachama juu ya TGA ni nini na inaweza kuwa........ 23
5.3 Kuimarisha utoaji wa huduma wa TGA ........ 23
5.3.1 Utoaji wa huduma zinazowanufaisha wanachama ni uti wa mgongo wa TGA ........ 23
5.3.2 Wakulima wa Miti Mabingwa........ 24
5.3.3 Kuimarisha uwezo wa wakulima wa miti katika misitu ........ 25
6. MODULI ZA MAFUNZO YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MISITU........ 26

6.1 Utangulizi ... 26
6.2 Kuanzisha na kusimamia kitalu cha miti ... 26
6.2.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji ... 26
6.2.2 Mafunzo katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa ... 28
6.3 Uanzishwaji wa shamba ... 29
6.3.1 Uanzishaji wa mashamba mapya ... 29
6.3.2 Usimamizi wa maotea ... 29
6.4 Usimamizi wa shamba- palizi ... 29
6.5 Usimamizi wa mashamba - upogoaji ... 30
6.6 Usimamizi wa mashamba - kupunguzia miti ... 30
6.6.1 Mafunzo ya FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa ... 31
6.7 Usimamizi wa shamba- uvunaji ... 31
6.8 Usimamizi wa mashamba - ulinzi na udhibiti wa moto ... 32
6.8.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji ... 32
6.8.2 Mafunzo ndani ya FWITC - kwa ajili ya Wakulima wa Miti Mabingwa ... 33
6.9 Kulima miti kama biashara - bei ya mbao huundwa vipi ... 33
6.9.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji ... 33
6.9.2 Mafunzo katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa ... 34

7. VIAMBATISHO ... 35

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho cha 1: Mapendekezo kwa PFP-2 ... 35
Kiambatisho cha 2: Rejea ... 37
Kiambatisho cha 3: Miongozo na miongozo ya usimamizi wa misitu ... 38

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1: Viashiria vinatoa uelekeo wa afua za uimarishaji wa TGA ... 9
Kielelezo 2: Mchakato pendekezwa wa uimarishaji uwezo wa TGA ... 9
Kielelezo 3: Mikutano katika ngazi ya kijiji wakati wa uhamasishaji ... 16
Kielelezo 4: Kuanzishwa kwa TGA. ... 17

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 1: Hatua kwa ajili ya barabara ya ukuaji wa TGA ... 14
Jedwali la 2: Matakwa ya usajili kama CBO au ushirika ... 18
Jedwali la 3: Mafunzo juu ya uanzishwaji wa kitalu na usimamizi katika ngazi ya vijiji ... 27
Jedwali la 4: Mafunzo juu ya uanzishaji wa kitalu na usimamizi katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa ... 28
Jedwali la 5: Mafunzo juu ya uanzishwaji wa mashamba ... 29
Jedwali la 6: Mafunzo juu ya usimamizi maotea ... 29
Jedwali la 7: Mafunzo ya upaliliaji ... 30
Jedwali la 8: Mafunzo ya upogoaji ... 30
Jedwali la 9: Mafunzo ya kutibu ... 30
Jedwali la 10: Mafunzo uvunaji - kwa wajasiriamali ... 31
Jedwali la 11: Mafunzo uvunaji - kwa wajasiriamali ... 31
Jedwali la 12: Mafunzo juu ya kuzuia na udhibiti wa moto ... 32
Jedwali la 13: Mafunzo katika uundaji wa bei ya mbao ... 33

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| *TGA/ TGA* | *Tree Growers Association/ Kikundi cha Wakulima wa Miti* |
| *TGA* | *Vikundi vya Wakulima wa Miti* |
| *PFP 2* | *Private Forestry Programme-Phase 2 (Panda Miti Kibiashara- awamu ya 2)* |
| *TTGAU* | *Tanzania Tree Growers Association Union (Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania)* |
| *MNRT* | *Ministry of Natural Resources and Tourism (Wizara ya Maliasili na Utalii)* |
| *NFBKP* | *National Forest and Beekeeping Programme (Programu ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki)* |
| *HRBA* | *Human Right Based Approach (Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu)* |
| *MTG* | *Master Tree Growers (Mkulima wa Miti Bingwa)* |
| *FWITC* | *Forestry and Wood Industries Training Centre (Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu)* |
| *FTI* | *Forestry Training Institute (Taasisi ya Mafunzo ya Misitu)* |
| *Afua* | *Shughuli mbalimbali za makusudi zinazofanywa ili kuweza kuleta matokeo au kubadilisha hali iliyopo.* |
| *TFS* | *Tanzania Forest Services* |

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Muhtasari

"Mwongozo wa Uwezeshaji wa Uanzishwaji na Uimarishwaji wa Vikundi Vya Wakulima wa Miti" unakusudiwa kutoa mwongozo kwa mashirika na taasisi zenye nia ya kuwezesha makundi ya wakulima wa miti kuunda vikundi vya Wakulima wa Miti (TGA/VIWAMI/KIWAMI), na/au kuimarisha utendaji wa vikundi vya Wakulima wa miti vilivyopo tayari.

Mwongozo umeandaliwa ndani ya muundo wa mradi wa PFP-2 kama sehemu mojawapo ambayo mradi imejikita kurahisisha na kuwa na mfumo unaofanana katika utoaji wa huduma kwa Vikundi vya Wakulima wa Miti (TGA). Mwongozo huu utaipatia Panda Miti Kibiashara (PFP-2) mwelekeo katika kujihusisha na TGA na unakusudiwa kutumika kwa matumizi ya hivi punde ndani ya mradi. Madhumuni ya muda mrefu ni kwa Panda Miti Kibiashara (PFP-2) kuupeleka mwongozo huu kwa wizara husika kwa matumizi ya kitaifa.

Muundo wa mwongozo ni kama ifuatavyo:

- Sura ya 2 inatoa mfumo wa ujumla wa kutumiwa wakati wa kujihusisha na afua mbalimbali za kuimarisha ushirika wa wakulima wa miti nainaelezea kwa muhtasarikanuni nane muhimu za kutumiwa.
- Sura ya 3 inafafanua sifa za TGA imara na hivyo inatoa msingi wa kuweka malengo katika uimarishaji uwezo. Pia sura hii inatoa hatua lengwa za kutumika kupima ukuaji na kuweka shabaha zenye maelezo ya kina kwa ajili ya usaidizi.
- Sura za 4 na 5 zinafafanua afua pendekezwa katika kusaidia vikundi vya wakulima wa miti (TGA). Sura moja inajikita kwenye uwezeshaji wa uanzishwaji wa TGA na wakati sura nyingine inajikita katika afua mbalimbali za kuimarisha TGA zilizopo.
- Sura ya 6 inafafanua moduli mahususi za mafunzo zinazopendekezwa katika usimamizi wa mashamba ya miti ili kuimarisha vyote: utoaji huduma kwa TGA na uwezo wa wakulima wa miti wa kusimamia na kuyatumia mashamba yao ya miti.

Mwongozo huu uliandaliwa katika kipindi cha Novemba - Disemba 2020 kupitia mchakato shirikishi uliohusisha timu ya Pandamiti Kibiashara (PFP-2) na vile vile Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU) na wataalamu kutoka Halmashauri za wilaya hasakutoka Njombe na Makete. Wakati wa maandalizi, nyaraka1 nyingi za muhimu zilipitiwa. Mwongozo huu ulithibitishwa na kupitishwa/kuasiliwa katika warsha ya wadau iliyofanyika tarehe 8 Desemba, Mafinga.

## 1.2 Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU)

Vikundi vya kwanza vya Wakulima wa Miti (TGA) vilianzishwa nchini Tanzania mnamo 2009 kupitia uwezeshaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) kupitia programu ya kitaifa ya Misitu Asilia na Ufugaji wa Nyuki (NFBKP). Kupitia uwezeshaji unaotokana na afua mbali mbali zinazofadhiliwa, ikiwemo Panda Miti Kibiashara awamu ya kwanza, Umoja wa Ulaya kupitia kampuni ya Green Resources Limited na Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU), idadi ya vikundi vya Wakulima wa Miti vimeongezeka na inakadiriwa kuwa kwa sasa vinakaribia 150 kwa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania.

Katika muktadha wa Tanzania, Vikundi vya Wakulima wa Miti ni shirika lisilo la kiserikali linaloundwa na wakulima wa miti katika ngazi ya kijiji ili liwasaidie katika ukulima wao wa miti. Uanachama katika Kikundi hiki ni wa hiari na wakulima wa miti wenyewe wanaamua ama wawe wanachama au la!

TGA inawanufaisha wanachama kupitia huduma anuai za usimamizi wa misitu, masoko vile vile kuzungumza na kutenda kwa niaba ya wanachama wake. Ingawaje, kwa sasa TGA zilizopo zipo bado katika hatua za awali za safari ya ukuaji wao na zitahitaji kuendelea na kuimarika

[1] Nyaraka zilizopitiwa zimo katika Kiambatanisho 1 cha Rejea

zaidi ili kuwa na uwezo mkamilifu wa kuwapatia huduma wanachama wake na kujikimu zenyewe kama taasisi.

## 2. KANUNI ZA MSINGI KATIKA UWEZESHAJI WA UANZISHWAJI NA UIMARISHARIJI WA TGA

Inapendekezwa kwamba taasisi na mashirika yanayojihusisha na uwezeshaji wa uanzishaji na uimarishaji wa TGA kuziasili kanuni msingi zilizoorodheshwa na kufafanuliwa hapa chini. Kanuni msingi hizi zinatoa mfumo wa jumla kwa ajili ya usaidizi ulioelezewa katika sura za 4 - 6.

### 2.1 "Utayari wa kutaka kuwa na ushirikiano" ndiyo msingi wa kuanzishwa kwa TGA

Kanuni ya msingi ya kuwawezesha wakulima wa miti kuanzisha TGA ni kwamba baina ya wakulima wenyewe iwepo nia thabiti ya kujumuika katika ushirika baina yao wenyewe katika masuala ya kilimo cha miti. "Utayari wa kutaka kuwa na ushirika" unamaanisha kwamba wakulima wa miti wanaanzisha TGA kwa hiari.

Jukumu la mwezeshaji ni kuwasaidia wakulima wa miti kuja pamoja, kuunda jukwaa ambalo wanaweza kujadili changamoto zao za kijamii na kiuchumi zinazohusiana na kilimo chao cha miti. Mwezeshaji anapaswa kuwasikiliza na kujifunza na kutokana na usaidizi huu wakulima wa miti wapate kuona fursa ya kutatua changamoto zao. Mkazo wa kwanza kwa umuhimu wa uwezeshaji, kwa pale yanapokuja masuala yote mawili uanzishwaji wa TGA na uimarishaji wa TGA zilizopo ni lazima uwe unaimarisha utumiaji wa rasilimali za ndani, uwawezeshe wakulima wa miti kuwa watawala wa hatima zao wao wenyewe.

Wakati wa kuwawezesha wakulima wa miti kuanzisha TGA, ukuzaji wa uelewa uwe ni kuhusu kutengeneza uelewa baina ya wakulima wa miti juu nini maana ya TGA na jinsi inavyoweza kuwa jukwaa/daraja la kutatua changamoto na kuchuma fursa zilizopo kwenye kilimo chao cha miti. Ukuzaji wa uelewa pia unahitaji kujumuisha kile kinachohitajika kuyafanya manufaa ya kikundi kuwa halisia (yaani Uhitaji wa TGA kukua) na si kuibua matarajio hewa ambayo baadaye yanaweza kuwakatisha tamaa yasipofikiwa.

Kuna hatari kwamba uwezeshaji, badala ya kuimarisha uelewa wa matumizi rasilimali za ndani kama suluhisho, ukatengeneza matarajio baina ya wakulima wa miti kwamba manufaa watakayoyapata yatatoka kwa mwezeshaji. Kisha hii inaweza kuwa motisha ya kuanzisha TGA, na sio uelewa thabiti wa manufaa ambayo TGA inaweza kuwapatia kwa kitambo cha muda mrefu. Hatari hii inatakiwa kusimamiwa kwa uangalifu. Uwezeshaji unahitaji kuepuka kuja na "vifurushi" ambavyo vitafanyika kama motisha ya nje kwa wakulima wa miti kujiunga katika TGA.

Kujihusisha na uwezeshaji wa uanzishaji wa TGA inahitaji taasisi inayowezesha kuelewa "barabara ya/muelekeo wa maendeleo" ya TGA, na kwamba kuanzishwa kwa TGA ni mwanzo tu. Hivyo, lipo hitaji la kujihusisha zaidi ya kupata usajili wa TGA pekee, kuiimarisha taasisi kukua katika uelekeo wa kuwa na uwezo wa kujikimu yenyewe kupitia uhamasishaji wa utumiaji wa rasilimali za ndani ya TGA.

### 2.2 Sehemu ya kuanzia katika kijiji ni kwenye TGA iliyopo au vikundi vya wakulima wa miti

Inapendekezwa kwamba sehemu ya kuanzia unapojihusisha na uanzishaji wa TGA katika kijiji ni kwanza kwa kutambua vikundi vilivyopo vya wakulima wa miti au TGA. Kama tayari vipo basi hatua ya pili ni kuvichambua (shughuli zao, muundo, changamoto n.k) kutathmini ikiwa vinaweza kuwa msingi wa TGA jumuishi katika kijiji. Pendekezo hili linajikita katika kanuni ya "utayari wa kutaka kuwa na ushirika" na mantiki ya kujenga juu ya kile kilichopo tayari katika ngazi ya kijiji.

Ikiwa tathmini inahitimisha kuwa TGA iliyopo au kikundi cha wakulima wa miti kina uwezo wa kukua, kutumia njia jumuishi ya kupokea wanachama wapya (kama vile wakulima wa miti watakaopenda wa ndani ya kijiji), uanzishwaji na mchakato wa kuimarisha TGA utajengwa juu ya kikundi au TGA iliyopo tayari. Ikiwa hitimisho la tathmini litakua tofauti, kutokana na kanuni za Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu (HRBA) na ujumuishi, uwezeshaji wa uanzishwaji wa TGA utaendelea sambamba na vikundi vilivyopo au TGA, na hivyo kuweza kupelekea kuwa na zaidi ya kikundi kimoja (au TGA) ndani ya kijiji.

## 2.3 Kuimarisha TGA ni kuhusu kikundi.

Falsafa iliyo nyuma ya wazo la TGA ni kwamba wakulima wa miti wanakuwa na kikundi chao wenyewe kinachowapatia huduma, vile vile kuwapa nguvu kupitia shughuli za paamoja na sauti ya pamoja (mf. katika masoko ya mbao). Hivyo kuwaimarisha wakulima wa miti kuwa watawala wa hatima zao. Kuimarisha TGA inamaanisha kuimarisha uwezo wa taasisi kutoa huduma hiyo, yaani kuimarisha taasisi (TGA) kuwa na uwezo wa kutoa huduma bora kwa wakulima wa miti (wanachama wa TGA) ili wanufaike zaidi na kilimo chao cha miti.

Kwa hiyo, kuna tofauti kati ya uimarishaji wa kitaasisi (TGA) na kuwajengea uwezo wakulima wa miti (wanachama wa TGA). Kuwafundisha wakulima wa miti usimamizi wa misitu si uimarishaji wa kitaasisi, mpaka pale ambapo uwezo wa TGA wa kutoa huduma hiyo hiyo umeimarishwa kwa wakati mmoja.

Ni muhimu kuelewa kikamilifu kuwa iwapo lengo ni kuimarisha TGA, hii inamaanisha kuwapo na hatua mahususi ambazo kupitia hizo uwezo wa shirika unajengwa. Hii inajumuisha yote mawili uwezo wa TGA kusimamia masuala yake (utawala na usimamizi) na kujenga uwezo wake wa kutoa huduma kwa wanachama wake. Kwa kuwa wanachama wa TGA ni wakulima wa miti, utoaji wa huduma utajikita katika mambo yanayohusiana na misitu.

## 2.4 Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu(HRBA) na ujumuishishwaji inatoa mfumo

Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu (HRBA) ni mbinu kuu katika maendeleo. Hivyo, njia hii inatoa msingi pia kuhusiana na uanzishwaji na uimarishaji wa TGA.

Afua za kuwezesha uanzishaji na uimarishaji wa TGA zinahitajika kuwa:


- Kuwa na uwezo wa kuwafikia wakulima wote wa miti katika kijiji. Hii inamaanisha kuwa TGA vinavyosaidiwa vinahitaji kuwa jumuishi katika suala la kuruhusu wakulima wa miti kujiunga navyo na hivyo kuruhusu wakulima wote wa miti kunufaika kwa usawa katika kupata huduma zinazotolewa ndani ya TGA.
- Kutumia njia isiyobaguzi na iliyojumuishi, inayotoa nafasi kwa wakulima wote wa miti kunufaika.
- Hususani, kuhusiana na uimarishaji wa utawala ndani ya TGA, inajumuisha afua mbalimbali ambazo zinawawezesha wanachama wenye mahitaji maalumu na walio fukara zaidi wakiwamo wanawake.
- Kukuza uwazi, uwajibikaji na usawa ndani ya TGA. Hivyo, kuchochea utoaji wa huduma ndani ya TGA unaotoa majibu ya mahitaji ya wanachama wengi walio ndani ya TGA kwa kadri iwezekanavyo, na sio kwa wanachama wenye nguvu kubwa pekee.

## 2.5 Viashiria vinatoa uelekeo kwa ajili ya uimarishaji wa TGA

Viashiria ni sifa za TGA imara. Viashiria hivi ni pamoja na namna TGA inavyoendesha shughuli zake (utawala na usimamizi) vile vile utoaji wake wa huduma kwa wanachama wake.

Viashiria hivi vinatoa uelekeo wa maendeleo ya TGA na hivyo vinaweka shabaha kwa afua/shughuli mbalimbali za uimarishaji wa TGA. Pia zinatoa mwongozo katika tathimini ya mahitaji ya kujengewa uwezo na upangaji wa afua mbalimbali za uimarishaji wa TGA. Ikiwa imeamuliwa kuweka hatua muhimu ikama sehemu ya kifurushi cha uimarishaji wa TGA, hapo pia viashiria vitakuwa na mashiko.


**Kielelezo 1: Viashiria vinatoa uelekeo wa afua za uimarishaji wa TGA**




## 2.6 Mchakato ulioundwa vizuri na endelevu kwa ajili ya uwezeshaji wa TGA

Kuimarisha TGA si tukio la mafunzo ya siku moja. Badala yake, ni kulea ukuaji wa TGA kuelekea viashiria, uwezeshaji unahitajika kuwa shirikishi, wenye mchakato ulioundwa vema na endelevu. Mchakato wa uimarishaji wa uwezo unapendekezwa kuanza na tathimini ya mahitaji ya kiuwezo na kutokana na tathimini kuwe na maandalizi shirikishi ya mpango wa kujenga uwezo kwa kila TGA. Mpango wa kujenga uwezo umilikiwe na TGA husika.

**Kielelezo 2: Mchakato pendekezwa wa uimarishaji uwezo wa** TGA




Uimarishaji uwezo unapendekezwa kutumia njia tofauti tofauti (kwa mfano warsha za mafunzo, malezi-ushauri ya vitendo, ziara za kutembeleana, misitu ya mfano) vile vile kuendelea na hatua za ufuatiliaji na hatua za marekebisho pale inapolazimu. Zaidi sana, inapendekezwa kwamba mbinu kamilifu itumike katika uimarishaji uwezo wa TGA ikiwemo kujenga uwezo juu ya usimamizi na utawala na utoaji huduma vile vile kuwapa wanachama uwezo wa kushiriki katika kufanya maamuzi ya TGA na kuuwajibisha uongozi.

Msaada wa kuwezesha ukuaji wa TGA unategemeana na kuwepo kwa kujidhatiti thabiti baina ya wakulima wa miti wa kutaka kuwa sehemu ya shirika na kuchangia maendeleo yake. Ikiwa kujidhatiti hakutakuwepo na hatua za kuongeza uelewa zikashindwa kuleta kujidhatiti kunakohitajika, kuna haja ya kuwa na chaguo la kusitisha msaada wa uimarishaji kitaasisi wa TGA. Hii haina maana kuwa hatua za uimarishaji uwezo zinazoelekezwa kwa wakulima wa miti na usimamizi na matumizi ya mashamba yao ya miti zitasitishwa.

## 2.7 Uhalisia wa TGA utawale usaidizi na ujuzi unaojitosheleza baina ya wawezeshaji ni msingi

Hatua za uimarishaji zinahitajika kutokana na uhasilia uliopo ndani ya TGA pindi linapokuja suala la kiwango cha ujuzi na uelewa. Hii inajumuisha vyote kile kinachotakiwa kutimizwa (mf. maudhui katika mpango wa TGA, ukubwa wa utoaji wa huduma unaotarajiwa) na maudhui na maelezo ya machapisho yaliyotumika (mf. kiwango cha kusoma na kuandika baina ya wanachama wa TGA)

Kuwezesha uanzishwaji na uimarishaji TGA inahusisha kuundwa kwa majukwaa kwa ajili ya wakulima wa miti kuja pamoja, kuimarisha uhamasishanaji baina ya wakulima wa miti na kugeuza fikra ili kuchuma fursa na kutatua changamoto. Hivyo, uwezeshaji unahitaji ujuzi na maarifa kuhusu mbinu za kuiwezesha jamii na zinazojikita katika haki za binadamu (HRBA). Mwezeshaji anahitaji kuelewa dhana ya TGA hususani falsafa iliyo nyuma ya TGA, hatua za kuunda TGA, kile TGA inachoweza kuwapatia wakulima wa miti sambamba na fursa na changamoto za kukifanya TGA kusimama na kimarika.

Kwa kuongezea juu ya "ujuzi laini" uliofafanuliwa hapo juu, ili kuimarisha TGA katika utoaji huduma, mwezeshaji anahitaji ujuzi wa kiufundi unaohusiana na misitu na kuongeza thamani ya mti.

Kabla ya kwanzaa shughuli katika vijiji, inapendekezwa kwamba ujuzi na uelewa utathiminiwa miongoni mwa wawezeshaji na kufanyika kwa uimarishaji uwezo kama italazimu kwa yote mawili linapokuja suala la wafanyakazi wako na watoa huduma wenye uwezekano wa kuhusishwa.

### 2.8 Ushirikiano na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU) na watoa huduma wengine ili kukuza uendelevu

Halmashauri ya Wilaya ni taasisi ya serikali iliyo na mamlaka muhimu katika uanzishwaji wa TGA na uimarishaji katika ngazi ya wilaya. Mamlaka ya halmashauri ya wilaya ni pamoja na misitu na maendeleo ya jamii. Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) ina jukumu la uundaji na utekelezaji wa sera na sheria za misitu nchini.

Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania (TTGAU[2]) ni shirika mwavuli la TGA. Mamlaka ya TTGAU ni kukuza maslahi ya wakulima wa miti ambao wanaushirika katika TGA ambavyo ni wanachama wa TTGAU.

Kulingana na mamlaka yake, inapendekezwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ihusishwe na upatikane ushauri kutoka kwao wakati wa kuwezesha uanzishaji na uimarishaji wa TGA. Ili kukuza uendelevu wa afua katika ngazi ya chini inapendekezwa kuanzisha ushirikiano wa karibu na Halmashauri za Wilaya na TTGAU. Pia inapendekezwa ushirikiano huo ujengwe juu ya mpango na ushirikishanaji wa taarifa sawa na makubaliano, kupanga na kutoa taarifa, kupanga mipango na mfumo wa kuripoti vile vile kuainisha mgawanyo dhairi wa majukumu na wajibu.

Kama ilivyoainishwa katika sura za 4 - 6, msaada wa uanzishaji na uimarishaji wa TGA unagusa maeneo tofauti ya masuala ya msingi na afua zinazofadhiliwa zitakazohitajika kupitishwa/kuasiliwa kuendana na kiwango cha ujuzi na uelewa uliopo katika ngazi ya kijiji.

[2] TGA ina fursa ya kuomba unachama kwenye TTGAU na uanachama ni hiari.

## 3. VIASHIRIA - SIFA ZA TGA IMARA

Sifa za TGA imara ni pamoja na kuendesha shughuli zake (usimamizi na utawala) na huduma kinazotoa kwa wanachama wake na pia kufuata muundo wa kisheria. Katiba ya TGA hutoa muundo wa kisheria kwa ujumla na hivyo kutoa fursa na/au kuweka mipaka ya kiutendaji ya TGA. Wakati huo huo pia TGA imara inazingatia miongozo iliyowekwa katika katiba yake.

TGA imara ina nguvu linapokuja suala la utoaji huduma na ukubwa wake, kushughulikia mabadiliko katika mazingira ya kiutendaji na mahitaji yaliyopo miongoni mwa wakulima wa miti, kazi ya pili inamaanisha kuwakaribisha wakulima wapya wa miti kwenye kikundi. Mfumo kwa ajili ya TGA imara hutokana na katiba yake (mf. kuwa jumuishi) na mipango yake (ramani ya wanakokuendea na uelekeo).

Viashiria vilivyopendekezwa vimeorodheshwa na kufafanuliwa katika sura za hapo chini. Ni muhimu kutambua kwamba viashiria vinavyoelezea TGA imara ni shabaha za juu sana. Tukiwa na pointi ya kuanzia, barabara ya kuvifikia viashiria vyote inaweza kuwa shabaha ya juu sana kwa TGA nyingi. Katika sura ya 3. Hatua 3 muhimu zimependekezwa kuongoza uwezeshaji wa maendeleo ya TGA.

### 3.1 Utawala na Usimamizi

#### 3.1.1 Usajili na nyaraka za uanzilishaji

***Kiashiria: katiba ya TGA***

TGA ina katiba ambayo hutoa mfumo wa jumla wa utendaji na utoaji huduma. Pia huamua ni nani anayeweza kuwa mwanachama wa TGA na hivyo kuamua kiwango cha ujumuishi wa TGA. TGA imara siyo tu ina katiba nzuri lakini pia inaifuata katiba hiyo. Kwa hiyo, wakati wa kutathmini TGA, katiba ni nyaraka muhimu ya rejea.

Katiba ya TGA iliyoandaliwa vizuri inajumuisha (ukiacha jina na anwani): i) mwelekeo (malengo, dira na dhima), ii) uteuzi wa wanachama, iii) mwongozo kwa uongozi na wanachama (kazi na majukumu, taratibu za uchaguzi) na iv) usimamizi (mikutano, ada, usimamizi wa fedha, utoaji ripoti), v) masuala ya jinsia.

***Kiashiria: Usajili***

TGA inasajiliwa[3] ama kama Shirika la Kijamii (CBO) kwenye Halmashauri ya Wilaya au kama Chama katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Usajili ni sharti la mwanzo ili TGA kutambuliwa rasmi na mamlaka kama taasisi halali kisheria na hivyo kuwa na uwezo wa kufungua akaunti ya benki au kujihusisha katika biashara na kununua na kuuza.

#### 3.1.2 Uongozi, mikutano na ofisi

***Kiashiria: Uongozi na wanachama waliowezeshwa***

TGA ina uongozi uliochaguliwa kama ilivyoainishwa kwenye katiba unaojumuisha angalau Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina. Uongozi huchaguliwa kama ilivyoainishwa katika katiba na chaguzi ni huru, za kiungwana na za haki. Wanachama wanatambua kwa kina haki zao na wanapewa nguvu ya kuuwajibisha uongozi.

Uongozi imara na wanachama waliopatiwa nguvu ni moja ya nguzo muhimu kwa TGA imara. Kwa hivyo, uongozi imara na wanachama waliopewa nguvu kwa kiasi fulani itaamua kama TGA itaweza kufikia viashiria vingine.

[3] Kuweza kuwa mwanachama wa TTGAU, TGA inahitaji kuwa imesajiliwa kama chama ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

***Kiashiria: Mikutano***

Mikutano ya mara kwa mara kufanywa. Mfululizo wa chini wa idadi ya mikutano utakuwa ule ambao umeainishwa katika katiba, yaani mikutano ya Mkutano Mkuu na ya Kamati Tendaji. Wanachama wanaarifiwa juu ya mikutano inayokuja mapema pamoja na kuarifiwa ajenda, hivyo kuruhusu ushiriki sawa baina ya washiriki. Mikutano inafanywa katika mazingira ambayo yanahimiza wanachama wote kupaza sauti zao. Muhtasari inaandaliwa na kupitishwa katika mkutano unaofuatia. Muhtasari inahifadhiwa kwenye ofisi ya TGA.

***Kiashiria: Ofisi.***

TGA ina ofisi ya masijala ambayo inakuwepo kama anwani ya kuifikia TGA husika. Ofisi ya masijala inajumuisha vifaa vya usimamizi wa fedha na mali (makabati yanayoweza kufungwa, sanduku la zana na vifaa) pamoja na samani za lazima kwa uongozi kutekeleza majukumu yao na kufanya mikutano.

### 3.1.3 Fedha na usimamizi wa mali

***Kiashiria: Usimamizi wa fedha***

TGA ina akaunti ya benki yenye taratibu zote za kiuhasibu na utunzaji kumbukumbu za fedha ikiwamo taratibu za kuidhinisha matumizi ya fedha ("hundi na salio"). Ripoti ya fedha inatolewa kwa wanachama kama katiba inavyoelekeza. Ukaguzi[4] wa fedha kutokea nje unafanywa kila mwaka na uonyesha usimamizi mzuri wa fedha.

***Kiashiria: Usimamizi wa mali na utunzaji wa kumbukumbu***

Mali za TGA zinarekodiwa katika orodha ya mali ambayo inatunzwa ofisini. Orodha ya mali inahuishwa angalau mara mbili kwa mwaka. Mali zinazohamishika (mf. zana) zinatunzwa ofisini huku kukiwa na utaratibu mzuri kwa ajili ya kurekodi uazimishaji/ukodishaji wa mali hizo kwa wanachama.

Nyaraka za TGA kama vile katiba, daftari la usajili wa wanachama, mipango, ripoti, muhtasari ya mikutano, ripoti za shughuli zinatakiwa zihifadhiwe ndani ya kabati linalofungwa ofisini. Uhifadhi unatakiwa uwe mzuri unaoruhusu kuipata nyaraka yeyote kwa urahisi.

***Kiashiria: Ada ya Uanachama***

Wanachama wa TGA hulipa ada zao za uanachama

### 3.1.4 Mipango na taratibu za kupanga mipango

***Kiashiria: Mipango***

TGA iendelee kuwa katika mfumo wa kupanga mipango ikiwemo mipango ya utendaji ya mwaka na mipango ya kimkakati. Mipango inawakilisha uhalisia wa TGA yanapokuja masuala yote mawili ya maelezo na madhumuni ya kufikia lengo. Mipango inaonesha picha ya wazi ya huduma zinanazohitajika na fursa za kuwapatia manufaa wanachama vile vile kutoa dira ya baadaye. Endapo TGA itakuwa inatekeleza miradi maalumu, mipango mahususi iandaliwe kwa ajili ya miradi hii. Mipango ni ramani ya kuiendea ya utoaji huduma ikijumuisha shughuli, rasilimali na ratiba, pia na namna ya kuripoti.

***Kiashiria: Taratibu za upangaji mipango***

TGA imeainisha taratibu dhahiri za namna ya kuandaa mipango ya mwaka na mipango mikakati. Taratibu zinafuatwa, na njia shirikishi zinatumiwa kuhakikisha ujumuishwaji wa wanachama wote katika mchakato wa kupanga mipango.

---

[4] Ofisi ya Halmashauri ya ushirika inaweza kutumika kwa ajili ya makusudi haya

### 3.1.5 Ushirikishanaji taarifa

***Kiashiria: Ripoti***

Ripoti zinaandaliwa kuendana na matakwa yaliyo ndani ya katiba ya TGA, sheria na uanachama ndani ya mashirika. Ripoti hizo zinajumuisha ripoti za ndani na nje. Mwisho ni pamoja na ripoti kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa TTGAU (endapo ni mwanachama)

Ripoti za ndani ni ripoti kwa Kamati Tendaji na pia kwa wanachama na hujumuisha angalau ripoti za mwaka na ripoti za robo mwaka za mali na fedha. Ripoti zinataarifu juu ya shughuli zilizofanywa na TGA na zinaangazia maendeleo yaliyopatikana kulinganishwa na mipango. Ripoti hizi ni namna kuu ya kushirikisha taarifa na mawasiliano na inawawezesha wanachama kuhabarika kwa taarifa za kutosha juu ya shughuli za ndani ya TGA.

***Kiashiria: Ubao wa Matangazo***

Ubao wa matangazo unatumika ndani ya kijijini kwa ajili ya kupeana taarifa. Kwenye Ubao wa matangazo TGA inatoa habari juu ya ratiba za mikutano na matukio yajayo.

***Kiashiria: Mfumo wa Jumbe Fupi (SMS)***

Taarifa itasambazwa ndani ya TGA kupitia mfumo wa Jumbe Fupi kuwafikia wanachama wote. Mfumo wa ujumbe mfupi utakuwa mbadala wa ubao wa matangazo na utatoa taarifa juu ya matukio yajayo, vile vile taarifa zinazohusiana na misitu. Mfano: taarifa za masoko ya mbao

## 3.2 Utoaji huduma kwa wanachama

### 3.2.1 Utoaji huduma na utaratibu wa kutoa mrejesho

***Kiashiria: Utoaji wa huduma***

Mipango ya TGA itatekelezwa kwa namna ya utoaji huduma kwa wanachama wake. Wanachama wote wanapewa fursa sawa za kupata huduma. Utaratibu wa kutoa mrejesho kuonyesha kama wanachama wanaridhishwa na huduma kuhusu upana wa huduma, ubora na gharama za huduma zitolewazo.

Utoaji wa huduma unafanywa kupitia wafanyakazi/wanachama au kupitia watoa huduma. TGA iweke rekodi ya watoa huduma wanaoweza kutumiwa.

***Kiashiria: Utaratibu wa kutoa mrejesho***

TGA inaendesha mfumo unaoruhusu washiriki kutoa mrejesho juu ya huduma inayotolewa na TGA na pia kupendekeza huduma mpya. Mrejesho ushugulikiwe na kuwasilishwa mara kwa mara katika mikutano ya wanachama. Utaratibu wa kupokea mrejesho hutoa mwongozo ili kuboresha ubora wa huduma vile vile kusaidia kuanzisha huduma mpya ndani ya TGA.

***Kiashiria: Uendelevu wa utoaji wa huduma***

Utoaji wa huduma huiingizia kipato TGA ambacho hukiwezesha kikundi kutoa huduma kwa wanachama wake na kuendeleza usimamizi wa kikundi.

## 3.3 Hatua muhimu - Taarifa kuongoza ukuaji wa TGA kufikia viashiria

Lengo la uimarishaji uwezo ni kuwezesha ukuaji wa TGA kufikia viashiria. Jedwali kwenye ukurasa unaofuata linapendekeza hatua za kupima ukuaji kwa kila kiashiria. Madhumuni ya hatua zilizopendekezwa ni kupima maendeleo kuelekea kuvifikia viashiria. Kwa mfano, kuna hatua tatu za kiashiria cha usimamizi wa fedha, ya kwanza inahusiana na kuwapo na taratibu (akaunti ya benki na utunzaji wa vitabu vya kiasibu). Baada ya kufikia hatua hii, shabaha inayofuata ni utendajikazi wa mfumo unaopelekea utoaji wa ripoti za kifedha. Shabaha namba 3 ni kuwa na ukaguzi wa nje unaoonyesha usimamizi mzuri wa fedha.

Ufuatiliaji wa mara kwa mara utatoa taarifa juu ya uboreshaji wa utendaji na upangaji wa afua zinazofadhiliwa zikazowekewa mpango katika mipango ya robo mwaka na/au mipango ya mwaka.

**Jedwali la 1: Hatua kwa ajili ya barabara ya ukuaji wa** TGA

| **Kiashiria** | **Hatua lengwa** | **Maoni** |
|---|---|---|
| Usajili wa TGA | TGA inasajiliwa | |
| Uongozi na uwezeshaji wa wanachama | Viongozi wa kudumu wanachaguliwa | |
| | Kuchaguliwa tena kwa viongozi kunafanywa kulingana na katiba | Hatua hii ifuate ratiba za uchaguzi mpya |
| Mikutano | Mikutano Mikuu na ya Kamati Tendaji inafanyika kama katiba inavyoelekeza | |
| | Agenda and minutes distributed<br>Ajenda na muhtasari inasambazwa | |
| Ofisi | Uanzishaji wa ofisi za TGA | |
| Usimamizi wa fedha | Akaunti ya benki inafunguliwa, kuwekwa kwa taratibu za uhasibu na mifumo ya utunzaji wa fedha taslimu | |
| | Ripoti za fedha zinaandaliwa kulingana na katiba na kutolewa/kuwasilishwa kwa wanachama | |
| | Ukaguzi wa nje kunafanywa kila mwaka | |
| Usimamizi wa mali na utunzaji wa kumbukumbu | Mali zinarekodiwa na orodha ya mali hizo kuwepo | |
| | Orodha ya mali inahuishwa kila mwaka | |
| | Kuanzisha utunzaji wa nyaraka kwa vifaa vya kuhifadhia kwa ajili ya nyaraka zote za TGA. | |
| Members<br>Wanachama | Katiba inakaribisha washiriki wapya | |
| | Idadi ya wanachama katika TGA ni 50% ya wakulima wa miti ndani ya kijiji | |
| | Idadi ya wanachama ni 75% ya wanachama waliopo ndani ya kijiji | |
| Mipango na utoaji wa huduma | Mpango wa kila mwaka wa shughuli (AOP) ulioandaliwa kuongoza utoaji wa huduma | Hatua za kuviifikia viashiria vilivyo kwenye mipango na utoaji wa huduma viunganishwe kwa kuwa vina uhusiano wa karibu |
| | Utendaji unafanyika kwa kiwango fulani sawa sawa na Mpango wa Mwaka wa Shughuli au mpango unaofanania Mpango wa Mwaka wa Shughuli. | |
| | AOP, or similar is prepared for year 2<br>Mpango wa Shughuli wa Mwaka, au kinachofanana na mpango wa shughuli unaandaliwa kwa muda miaka miwili | Hatua kwa ajili ya utoaji huduma zinahitajika kuhuishwa wakati Mpango wa Mwaka wa Shughuli, unaofanana na huo unapoandaliwa kwani maelezo yatatoka kwenye hizo |
| | Utendaji unafanyika kwa kiwango fulani sawa sawa na Mpango wa Mwaka wa Shughuli au mpango unaofanania Mpango Mwaka wa Shuguli | |
| | Utoaji wa huduma unaingiza kipato kuiwezesha TGA kupanua huduma | |
| Ripoti | Ripoti zinaandaliwa kulingana na matakwa yaliyopo ndani ya katiba | |
| Mfumo wa taarifa/habari | Mfumo wa kidijitali uko tayari na unafanya kazi katika kushirikisha taarifa | |
| | Mfumo huu hutoa mara kwa mara habari mpya zenye uthamani zihusuzo uzalishaji kipato kwa ajili ya wakulima wa miti | |

## 4. KUWEZESHA UANZISHWAJI WA KIKUNDI CHA WAKULIMA WA MITI

### 4.1 Utangulizi

Utayari wa wapandaji wa miti kuungana ili wawe na umoja katika usimamizi wa mashamba yao ndio msingi wa uanzishwaji wa TGA. Jukumu la mwezeshaji litakuwa kuwapatia uelewa wakulima wa miti kuhusu faida za TGA na hivyo kuleta hamasa kuanzisha TGA. Uhamasishaji wa TGA unahitaji kudhibiti kwa umakini hatari ya wakulima wa miti kuanza kukubali manufaa yatokanayo na uwezeshaji wenyewe na hiyo ikawa motisha kwao kuanzisha TGA yao.

Sehemu ya kuanzia ni kwa kuanza na kile kilichopo ndani ya kijiji. Hivyo kwanza tunabaini TGA vilivyopo, kisha tunavihusisha na wakati huo huo tunavitathmini ili kuona kama vinaweza kutupa sehemu ya kuanzia katika uanzishwaji wa TGA jumuishi katika vijiji husika. Idadi[5] ya wanachama wa TGA inapendekezwa kutopungua wanachama 30.

Ni vema tujikumbushe kuwa uwezeshaji unahitaji muda, ujuzi na maarifa. Ujuzi unaohitajika ni pamoja na mbinu jumuishi za kuhudumia jamii kupitia Mbinu Zinazozingatia na Haki za Binadamu na uundaji wa vikundi. Hivyo, ili tuweze kuhamasisha uundaji wa TGA, mwezeshaji anahitaji kuwa na uelewa mpana TGA ni nini, manufaa yake ni yapi, fursa gani zinazopatikana na changamoto zinazoweza kujitokeza mpaka kufikia kipindi ambacho TGA iweze kusimama yenyewe na kujitegemea.

Mchakato mzima wa uwezeshaji wa kuanzisha TGA umeainishwa katika sura zinazofuata. Uwezeshaji unapaswa kuhakikisha kwamba mchakato wa uanzishwaji wa TGA ni shirikishi na jumuishi kwa wakulima wa miti wote, (yaani wanachama watarajiwa wa TGA) katika kijiji.

Kuna hatua mbili kuu katika uanzishaji wa TGA:

i. Uhamasishaji

ii. Kuanzishwa kwa TGA.

"Uhamasishaji" unalenga kuongeza ufahamu na uelewa baina ya wakulima wa miti kuhusu TGA ni nini na manufaa yanayoweza kupatikana kutokana na uanzishaji wa TGA. Endapo wakulima wa miti wataona kuna manufaa kuanzisha TGA, uwezesha utaendelea kutokea kwenye hatua ya uhamasishaji kwenda kwenye hatua inayofuata ya uanzishaji. Endapo wakulima wa miti hawakuvutiwa na kujiunganisha kwenye TGA, mchakato unaishia katika hatua ya kwanza ya uhamasishaji.

"Uanzishwaji" wa vikundi una lengo la kuwawezesha wakulima wa mti kuanzisha kikundi chao. Kazi inayofuata baada ya kuanzishwa kikundi ni kukisajiri kupitia mamlaka husika.

### 4.2 Hatua ya 1: Uhamasishaji

#### 4.2.1 Mikutano ya maandalizi kabla ya kujihusisha katika kijiji

***Kuwasiliana na taasisi muhimu***

Mwezeshaji anahitaji kuwa na taarifa za kutosha na kupata taarifa zote za lazima za kitaasisi na za mchakato. Miongoni mwa mengine mengi, Mwongozo unapendekeza mawasiliano na taasisi muhimu zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaaa, TTGAU, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na zingine kama hizo. Kupitia mashauriano haya mwezeshaji atapata taarifa juu ya TGA zinazoweza kuwepo katika kijiji husika na vile vile uwezekano wa afua zinazoendelea zinazohitaji kuzingatiwa katika uwezeshaji zaidi. Katika hatua hii mwezeshaji anapaswa kuzingatia uendelevu wa TGA itakayo anzishwa kwa kuhimiza ushirikiano mzuri na mchakato wa uwezeshaji wenye uwazi.

[5] TTGAU inapendekeza ukubwa wa TGA kuwa na wanachama 30 - 200. Kikomo cha juu kinazingatia uwezo wa utawala wa TGA zilizopo sasa. Endapo kuna wakulima wa miti zaidi ya 200 ndani ya kijiji TTGAU inapendekeza kuundwa TGA chache ndani ya kijiji hicho hicho.

*Mawasiliano na mamlaka zinazohusika*

Kabla ya uwezeshaji katika ngazi ya kijiji, inapendekezwa kuwa mwezeshaji ashirikishe mamlaka za serikali za mitaa (LGAs) ambazo zinajumuisha mamlaka za serikali za mikoa na wilaya. Katika kuwashirikisha Katibu Tawala Mkoa na Mkurugenzi wa Wilaya pamoja na idara husika (misitu na maendeleo ya jamii) zinataarifiwa juu ya nia ya uwezekano wa kuwezesha uundaji wa TGA miongonii mwa wakulima ndani ya kijiji husika. Msaada wa idara mbali mbali katika uwezeshaji katika kijiji unapangwa na kukubaliwa. Hivyo, matokeo ya kushirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ni ufahamu wa wazi na mchakato wa mbeleni uliokubaliwa pamoja na kazi na majukumu.

### 4.2.2 Mikutano katika ngazi ya kijiji

Inapendekezwa kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya kujihusisha katika kijiji. Kanuni bora ni kutumia angalau wiki moja katika kijiji. Utaratibu katika kijiji unaainishwa kwenye kielelezo hapa chini.

Ikiwa mkutano wa Kijiji, mkutano wa mwisho katika mchakato, unahitimisha kuwa kuna nia miongoni mwa wakulima wa miti kujiunga katika TGA, viongozi wa kijiji wataongoza kuorodhesha majina ya wakulima wa miti wanaopenda kujiunga na TGA. Inapendekezwa kuwa viongozi wa vijiji waandikie barua kwa kata, halmashauri ya wilaya na TTGAU kuwataarifu juu ya uamuzi na mchakato unaokuja mbeleni.

**Kielelezo 3: Mikutano katika ngazi ya kijiji wakati wa uhamasishaji**




*Mkutano katika ofisi ya Kata*

Uwezeshaji katika ngazi ya kijiji huanza na mkutano katika ofisi ya Kata. Lengo la mkutano huu ni kuarifu juu ya nia ya kuwezesha uwezekano uanzishwaji wa TGA miongoni mwa wakulima wa miti katika kijiji mahususi ndani ya kata.

*Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji*

Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji una lengo sawa na mkutano unaofanyika halmashauri ya wilaya, yaani kutoa taarifa juu ya nia ya kuwezesha uwezekano wa kuanzishwa kwa TGA miungoni mwa wakulima wa miti katika kijiji husika na kukubaliana juu ya mchakato wa mbeleni na kazi na majukumu. Kwa kuongezea, hii inatoa nafasi kwa serikali ya kijiji kuumiliki na kuongoza mchakato.

*Mkutano wa Kijiji*

Lengo la mkutano wa kijiji ni kuwapa taarifa wanakijiji kuwa kuhusishwa kwao katika ngazi ya kijiji kunaanzia ngazi ya kata. Wakati huo huo wanakijiji wanataarifiwa juu ya ratiba za kupatiwa uelewa katika mikutano ya vitongoji na mikutano ya mwisho ya kijiji.

*Kuongeza uelewa katika vitongoiji*

Kuongeza uelewa katika kila kitongoji ndiko ambapo uhusikanaji halisi na wakulima wa miti huanzia. Hapa uwezeshaji unachukua njia shirikishi na jumuishi katika kuwahusisha wakulima wa miti. Kiongozi wa kitongoji hufanya kazi na mwezeshaji katika kuongeza uelewa kuhusiana na TGA. Inapendekezwa kuwa siku 1 itengwe kwa ajili ya kuwahusisha wakulima wa miti kwa kila kitongoji na kwamba umakini mahususi uwekwe katika kuhakikisha kuwa makundi yote ya wakulima wa miti yanahusishwa na kusikilizwa.

*Mkutano wa Kijiji*

Kuongeza uelewa katika vitongoji hufuatiwa na mkutano wa kijiji. Kwenye mkutano wa kijiji, hitimisho kutokea kwenye mikutano katika vitongoji huwasilishwa na kujadiliwa zaidi. Ikiwa hakuna nia baina ya wakulima wa miti kuanzisha TGA yao, zoezi linahitimishwa, na uwezeshaji unakomea kwenye mkutano wa kijiji. Tena endapo mikutano katika ngazi ya kitongoji imeleta nia ya kuanzisha TGA, jambo hili litajadiliwa zaidi, maswali ya nyongeza yanayoweza kujitokeza yafafanuliwe na mchakato wa mbeleni wa kuanzisha TGA utolewe unafafanuzi.


## 4.3 Hatua ya 2: Uanzishwaji

Uwezeshaji wa uanzishwaji wa TGA ni kuhusu:

- Kutengeneza ufahamu zaidi na uelewa wa TGA ni nini na hasa juu ya matakwa ya viongozi na nini cha kutarajia kutoka kwa viongozi ndani ya TGA. Katika kuongeza uelewa wa mambo ya kijinsia yanaangaziwa ili kuhamasisha mtazamo wa usawa wa kijinsia katika uteuzi wa viongozi wa kijiji.
- Kuandaa katiba ya TGA pamoja na kukuza uelewa wa wanachama juu ya katiba ni nini, maeneo muhimu ambayo yanahitaji kuwa katika katiba na utengenezwaji shirikishi wa katiba. Uangalifu mahususi utolewe kwenye mbinu jumuishi katika kukaribisha washiriki kwenye TGA. Katiba ya mfano inaunda msingi wa uwezeshaji huu.
- Kusaidia wanachama katika uamuzi wao juu ya aina ya ipi ya shirika waanzishe (kawaida ni kikundi cha aina ya Shirika la Kijamii- CBO).
- Usaidizi wa kivitendo katika usajili, kuhakikisha kuwa uchelewaji na/au vizuizi vinavyoletelezwa na mfano kama nyaraka kutotosheleza vinaondoshwa.

Uanzishwaji wa TGA unakamilika pindi TGA imesajiliwa. Wakati wa mchakato wa uanzishwaji viongozi wa muda wanachaguliwa na TGA huanza kazi yake na uongozi wa mpito. Viongozi wa kudumu wa TGA iliyosajiliwa wanachaguliwa kulingana na masharti ya katiba, katika mkutano wa wanachama baada ya TGA kusajiliwa. Mchakato wa uanzishwaji wa TGA umeainishwa kwenye kielelezo hapa chini.

**Kielelezo 4: Kuanzishwa kwa TGA.**




*Mafunzo ya utawala*

Wakulima wa miti walioorodheshwa kwamba wana nia ya kujiunga na TGA wanapokea mafunzo kuwaongezea ufahamu na uelewa wa nini watarajie kutoka kwa kiongozi na nini inamaanisha kimajukumu kuwa mwanachama wa TGA. Mafunzo yanapendekezwa yawe ya kitambo cha siku 2.

*Uchaguzi wa viongozi wa muda wa TGA*

Baada ya mafunzo ya utawala wakulima wa miti "wanachama watarajiwa wa TGA" wanachagua uongozi wa mpito wa TGA inayoanzishwa. Inapendekezwa kwamba kwa ajili ya viongozi wa mpito watu wanne wachaguliwe; mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu na mweka hazina. Inapendekezwa kwamba umakini maalumu uwekwe katika kuzingatia ya mambo ya kijinsia katika uchaguzi wa viongozi wa mpito

***Uundaji wa katiba***

Uwezeshaji wa uundaji wa katiba ni pamoja na kuongeza uelewa vile vile kutoa msaada wa kivitendo katika uundaji wa katiba. Sehemu za msingi za kukuza uelewa na msaada wa kivitendo ni pamoja na katiba ni nini, vipengele tofauti vya katiba, aina tofauti za mashirika na uundaji wenyewe wa katiba. Hapa katiba ya mfano inatumika kwa msaada.

Inapendekezwa kutenga siku 2 kwa ajili ya uwezeshaji na uandaaji wa katiba. Kulingana na maamuzi ya hivi karibuni ndani ya TTGAU inapendekezwa kwamba katiba ya TGA pia ijumuishe mabadiliko ya tabia ya nchi, hatua za kuchukuliwa na utatuzi na ujumuishi wa kijinsia.

***Usajili***

Uwezeshaji wa usajili ni pamoja na kuongeza uelewa wa nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya usajili, mchakato wa usajili na machagulio tofauti ya muundo wa mashirika kwa ajili ya TGA. Usaidizi wa kivitendo unatolewa kwenye usajili wenyewe.

Matakwa ya usajili kama Shirika la Kijamii(CBO) au chama yameainishwa katika jedwali hapa chini. Kwa sasa, TTGAU inapendekeza TGA kujisajili kama vyama, kwani hiyo ni sharti kwa TGA kuweza kuwa wanachama katika TTGAU.

**Jedwali la 2: Matakwa ya usajili kama CBO au ushirika**

| Takwa | Usajili kama CBO | Usajili kama chama |
|---|---|---|
| Mamlaka ya usajili | Mamlaka ya Serikali za Mitaa chini ya Sheria ya Shirika lisilo la Serikali (Sura ya 56) ya 2019 | Taratibu za usajili wa vyama nchini Tanzania hutolewa chini ya Sheria ya Vyama, [cap. 337 R.E 2002] na marekebisho ya hivi karibuni ya Sheria zilizoandikwa (Marekebisho ya Ziada) (Na 3) Sheria ya 2019] |
| Nyaraka zinazohitajika | 1.Nakala ya orodha ya kidigitali na ya karatasi ya wanachama waanzilishi wasiopungua watano<br>2. Nakala ya kidigitali na ya karatasi ya katiba<br>3. Nakala ya kidigitali na karatasi za Wasifu wa viongozi / viongozi wanaoshikilia ofisi na picha mbili mbili za pasipoti za kila mmoja. | 1. Barua ya maombi itumwe kwa Msajili wa Vyama vya Kijamii.<br>2. Nakala 3 za Katiba ya Chama Sheria ndogo ndogo za Chama<br>3. Fomu ya SA namba 1 na 2 zote mbili zikiwa na nakala zake.<br>4. Muhtasari wa idhini ya kuanzisha Chama kilichotajwa ulio na orodha iliyo na majina kamili na saini za wanachama waanzilishi wasiopungua 10. (unaweza kuwasilishwa peke yake).<br>5. Maelezo ya binafsi ya viongozi /Wasifu wao(CV).<br>6. Picha za ukubwa wa pasipoti za viongozi.<br>7. Barua za utambulisho kutoka kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo itatakiwa kuwasilishwa kwenye ofisi za Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kuidhinishwa au Wizara Mama au Taasisi.<br>8. Nakala za Maombi zitaandaliwa 1 kwa kila idhinisho na itawasilishwa kwa Msajili, nakala nyingine 2 zitakuwa za shirika na Mwanasheria kwa ajili ya kumbukumbu)<br>9. Anwani kamili na eneo la kuifikia ofisi kuu ya shirika inapopatikana. |
| Muda | Mchakato huu ni mfupi ikiwa usajili uko kwa viongozi wa wilaya | Usajili ufanywa wizarani Dodoma na unaweza kuchukua muda, wakati mwingine hadi mwaka mmoja. |
| Gharama za usajili | Mamlaka ya Wilaya TSH 41,500<br>Mamlaka ya Mkoa TSH 56,500 | 150 000 TZS<br>TSH 150 000 |

| | | |
|---|---|---|
| | Kitaifa TSH 66,500 | |
| Upana wa shughuli | Unaweza kuwa wa wilaya, mkoa, kitaifa au kimataifa, kutegemeana na wapi chama kimesajiliwa. | Kufikia Sehemu kubwa zaidi |
| TTGAU | TGA iliyosajiliwa kama CBO hakikubaliki kuwa mwanachama wa TTGAU | Inakubaliwa kama mwanachama wa TTGAU |
| Shughuli za biashara | Haiwezi kufanya shughuli za biashara kwa ajili ya faida/ inaweza kushiriki katika biashara ya kijamii | Inaweza kushiriki katika shughuli za biashara kutengeza faida. |

## 5. UIMARISHAJI KIKUNDI CHA WAKULIMA WA MITI

### 5.1 Mfumo

Uimarishwaji TGA ni juu ya maendeleo ya kitaasisi na ni pamoja na kujenga uwezo wa kikundi kusimamia mambo yake (utawala na usimamizi) na pia kutoa huduma kwa wanachama wake. Kwa kuwa wanachama ni wakulima wa miti, huduma hizo zina uwezekano mkubwa wa kuhusika na misitu. Ni muhimu kutambua tofauti kati ya kujenga uwezo wa wakulima wa miti na kuimarisha kikundi (TGA).

viashiria (sura ya 3) vinatoa mwelekeo wa hatua za kuimarisha TGA. Inapendekezwa sana kwamba hatua hizo zitumie Mbinu Zingativu ya Haki za Binadamu na ujumuishi na kuhimiza TGA kuwaalika wakulima wote wa miti katika kikundi ili kunufaika na utoaji wa huduma wa TGA.

Kulea ukuaji wa TGA kufikia viashiria, inapendekezwa kuwa uwezeshaji uchukue mchakato ulioundwa vizuri na endelevu kuanzia kwenye mahitaji ya kiuwezo ikifuatiwa na mpango wa kujenga uwezo na afua za uimarishaji kwa kutumia njia tofauti tofauti.

### 5.2 Kujenga uwezo wa TGA juu ya utawala na usimamizi

Kuijengea TGA uwezo wa kuendesha shughuli zake ni pamoja na ujuzi na uelewa kuhusu utawala halisia, kufanya mikutano, mawasiliano na kushirikishana taarifa, uwezo wa uongozi na mitazamo ya wanachama juu ya majukumu yao, TGA ni nini na inaweza kuwa nini. Kwa hiyo mada za kujumuishwa kwenye kuimarisha uwezo wa utawala na usimamizi wa TGA ni pamoja na:

- Usimamizi wa fedha na mali ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kumbukumbu.
- Mikutano: kupanga, kuendesha na muhtasari.
- Kushirikishana taarifa: Ripoti, mifumo ya kushirikisha taarifa.
- Mipango na taratibu za kupanga mipango.
- Uongozi na wanachama

Kwa kuongezea kwenye ujuzi na uelewa, kujenga uwezo kunawezekana pia kujumuisha uboreshaji wa vitu na vifaa kwa ajili ya usimamizi (k.m vitu kwa ajili ya utunzaji rekodi za kihasibu, makabati ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka).

Kutoka kwenye mtazamo wa utawala uimarishaji wa TGA unahitaji kujumuisha hatua zote mbili kuimarisha uongozi kusimamia mambo na afua za kuwawezesha wanachama. Kuwawezesha wanachama ni pamoja na wao kuelewa kazi yao na jukumu lao kama wanachama vile vile haki yao ya kuwawajibisha viongozi.

Moja ya vizuizi vikuu vya ukuaji wa TGA kwa kawaida huwa ukomo kwenye maono ya nini kile TGA inaweza kuwa, jinsi ya kuandaa ramani ya sehemu kinachota kwenda ili kuifikia dira na jinsi ya kutekeleza ramani yenye uelekeo wa wnaotaka kwenda. Kwa maneno mengine, upangaji, mipango na utekelezaji. Upangaji unahitaji kuwa shirikishi na jumuishi, unaoruhusu wanachama wote kusikika sauti zao. Inapendekezwa kuwa uimarishaji wa uwezo juu ya mipango na upangaji vichukuliwe kama masuala tofauti (kama vile katika afua ya 3 kwenye orodha hapa chini).

Kuimarisha uwezo kunapendekezwa kuundwa katika aina kuu tatu za afua:

I. Kujenga uwezo wa uongozi uliochaguliwa kusimamia mambo ya TGA.

II. Kuwawezesha wanachama kuelewa haki zao, shughuli na majukumu yao.

III. Kuimarisha mitazamo ya viongozi na wanachama juu ya TGA yao ni nini na inaweza kuwa nini (mipango na upangaji).

### 5.2.1 Mafunzo mahusi kwa uongozi wa TGA

Kundi lengwa kwa ajili ya kuimarishwa uwezo ni viongozi waliochaguliwa kama ilivyoainishwa katika katiba ya TGA, yaani. mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu, mweka hazina na wajumbe wa Kamati Tendaji. Lengo ni kuongeza utawala bora wa TGA kupitia kuimarisha uwezo wa viongozi waliochaguliwa kutekeleza majukumu yao waliyopewa.

Inapendekezwa kuwa njia tofauti kutumiwa kuimarisha uwezo ikiwa ni pamoja na warsha maalumu za mafunzo, malezi-ushauri ya kivitendo na ziara za kujifunza za kutembeleana. Mwongozo huu unaelezea kimahususi mapendekezo juu ya matukio maalumu ya mafunzo kwa kila viongozi waliochaguliwa. Moduli za mafunzo zilizopendekezwa zimeelezewa hapo chini.

Mafunzo ya viongozi waliochaguliwa yanapendekezwa kufanyikia katika kituo maalumu (mf. katika ngazi ya wilaya au FWITC) na kujumuisha viongozi wa TGA kadhaa. Kwa mfano, makatibu 10 hadi 15 kutoka kwenye TGA waletwe pamoja mahali pa kufaa kwa ajili ya warsha ya mafunzo. Hii itaongeza ufanisi wa mafunzo, kuwezesha wanaojifunza kuzingatia mafunzo na pia kukuza kubadilishana taarifa na uzoefu baina ya TGA.

Mtoa huduma anayetoa mafunzo anahitaji kuwa na ujuzi mahususi juu ya masomo yanayohusika na uwezo uliothibitishwa wa kufanya mafunzo, itafaa ikiwa shirika lililojikita katika maendeleo ya taasisi na/au maendeleo ya biashara kwa njia zinazoendana na hali halisi na mahitaji ya wanaofundishwa.

***Moduli ya mafunzo: wenyeviti, katibu na wajumbe wa Kamati Tendaji***

Sababu za kupendekeza mafunzo ya wenyeviti na makatibu kwa sehemu wafanyiwe pamoja ni:

- Mfanano wa majukumu ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti na katibu.
- Uhitaji wa wao kushirikiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu yao ya TGA.
- Hitaji la uelewa wazi wa shughuli na majukumu yao tofauti.

Katika baadhi ya TGA katiba inafafanua Kamati Tendaji kujumuisha pamoja na wenyeviti, katibu na mweka hazina, wanachama wengine wawili. Inapendekezwa kuwa "wajumbe wengine wawili" wa Kamati Tendaji washiriki wakati wa siku moja ya mafunzo, pindi mada zinazowahusu ziko kwenye ajenda (mf. kuendesha mikutano).

Muda unaopendekezwa wa moduli ya mafunzo ni siku 4 na yatafanywa kwa sehemu wenyeviti na katibu wakia pamoja, ili wenyeviti washiriki siku 1 - 3 na katibu siku 1 - 4. Mafunzo yanapendekezwa kuzingatia maudhui yaliyomo kwenye katiba ya TGA vile vile utendaji wa kawaida katika vikundi vinavyofanya kazi vizuri kwa kuzingatia usimamizi na uongozi.

Mafunzo hayo yajumuishe mada zifuatazo:

- Uongozi katika TGA
- Kuandaa na kuendesha mikutano
- Mipango, Upangaji na utekelezaji
- Ripoti; maandalizi na uwasilishaji
- Ufuatiliaji wa shughuli za TGA
- Usimamizi wa migogoro na utatuzi
- Majukumu mahususi ya katibu; utunzaji wa rekodi, kuandika muhtasari, kutunza nyaraka

Wakati wa tathmini ya mahitaji, vifaa vilivyopo kwa ajili ya katibu vinaangaliwa. Sehemu ya uimarishaji wa uwezo itakuwa kujaza nafasi zinazowezekana katika vifaa na kuwapa makatibu nyenzo na vifaa vya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao. Zana za msingi za katibu inapendekezwa kuorodheshwa na kutayarishwa kwa usambazaji wakati wa mafunzo.

***Moduli ya mafunzo: Mweka Hazina***

Inapendekezwa kuwa mafunzo yajikite kwenye majukumu ya mweka hazina kama ilivyoainishwa katika katiba ya TGA. Muda uliopendekezwa wa moduli ya mafunzo ni siku 4.

Moduli ya mafunzo inapendekezwa kujumuisha mada zifuatazo:

- Usimamizi wa kifedha pamoja na: Sifa za usimamizi mzuri wa kifedha, usimamizi wa akaunti za benki, usimamizi wa hazina na fesha taslimu, uhasibu, utunzaji wa kumbukumbu na utayarishaji wa ripoti za kifedha.
- Upangaji mipango na upangaji bajeti.

Wakati wa tathmini ya mahitaji, vifaa vya hazina vitaangaliwa. Sehemu ya uimarishaji wa uwezo itakuwa kujaza nafasi zinazowezekana katika vifaa na kumpa mweka hazina nyenzo na vifaa vya kumwezesha kutekeleza majukumu yake. Zana za msingi za mhazini inapendekezwa kuorodheshwa na kutayarishwa kwa usambazaji wakati wa mafunzo.

### 5.2.2 Kuwawezesha wanachama wa TGA

Kundi lengwa kwa ajili ya uimarishwaji uwezo ni wanachama wote wa TGA. Kusudi ni kuongeza utawala bora na njia jumuishi katika TGA kupitia kuimarisha uwezo wa wanachama wa TGA kuelewa:

- Haki zao kama wanachama wa TGA na jukumu la uongozi na kwa kuzingatia hili waweze kuuwajibisha uongozi kwa matendo yao.
- Wajibu wa kuwa mwanachama wa TGA.

Mikutano ya siku moja ya uhamasishaji wa wanachama inapendekezwa kama afua kuu ya kuchukuliwa kuimarisha uwezo, itapendeza mikutano kufanywa karibu na Mkutano Mkuu wa TGA kuhamasisha ushiriki wa dhati katika Mkutano Mkuu. Kupanga ratiba na kutekeleza mikutano inahitaji kuruhusu ushiriki sawa na sauti za wote kusikilizwa. Njia yenye mikutano midogo (k.m mkutano katika ngazi ya kitongoji, mikutano mahususi kwa ajili ya wanawake) inaweza pia kutumika.

Mikutano ya kuimarisha uelewa wa wanachama inaweza kuwa ya kujirudia rudia kuimarisha utawala ikiwa inahitajika. Ufuatiliaji wa utendaji wa usimamizi wa TGA hutoa taarifa juu ya uhitaji wa afua za kujirudia rudia.

Mada ni sawa na za uongozi, lakini hazitakuwa za kina na badala yake zitazingatia hitaji la uelewa kutokea kwenye mtazamo wa mwanachama:

- Uongozi: Ni nini kinachotakiwa kudaiwa kutoka kwa kiongozi mzuri. Haki zangu kama mwanachama ni zipi na ni njia gani za kubadilisha uongozi ikiwa itahitajika.
- Usimamizi wa Fedha: upi nii usimamizi mzuri wa fedha na ni taarifa gani za kifedha itakayowasilishwa kwa wanachama.
- Mikutano: Mikutano iliyoainishwa katika katiba na nini kinapaswa kushughulikiwa wakati wa mikutano.
- Taarifa: ni taarifa gani zinayopaswa kushirikishwa kwa wanachama na ni njia gani za kushirikisha taarifa hizo.
- Ripoti za maendeleo: ni ripoti zipi zinatakiwa kutayarishwa na ni akina nani washirikishwe taarifa hizo pamoja na wanachama.
- Jinsia na Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu.
- Kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hatua zilizochukuliwa.

### 5.2.3 Mipango na Upangaji - kuimarisha viongozi na mitazamo ya wanachama juu ya TGA ni nini na inaweza kuwa.

Moja ya vizuizi vikuu kwa ukuaji wa TGA ni ufinyu wa maono juu ya kile TGA inaweza kuwa, jinsi ya kuandaa ramani ya kule kinakotaka kufika na kuitumia kufikia dira. Kwa maneno mengine, jinsi ya kuandaa mpango wa mwaka na mpango mkakati na mipango biashara na jinsi ya kuiweka kwenye utendaji.

Ingawa uongozi wa TGA unawajibika katika uundaji wa mwisho wa mipango na pia utekelezwaji wake, mchakato wa kukubaliana yatakayokuwemo kwenye mipango unahitaji kuwa shirikishi na jumuishi. Kwa hiyo, uimarishaji uwezo wa kupanga katika TGA unahitaji kujumuisha uongozi pamoja na wanachama.

Kuimarisha mipango na utekelezaji wa mipango ni mchakato endelevu ambapo uwezo unakua taratibu. Uwezeshaji unajumuisha uandaaji wa mipango na vile vile kuwapatia malezi ya kivitendo katika utekelezaji wa mipango hiyo. Kujenga uwezo juu ya usimamiaji na utawala (angalia sura za awali) na pia juu ya utoaji wa huduma (tazama sura ya 5 na 6) zimeunganishwa kwa karibu ili kuimarisha utekelezaji wa mipango.

Moduli maalum ya mafunzo ya uimarishaji wa uwezo wa upangaji wa mipango katika TGA inapendekezwa kuwa na muda wa siku 2 - 3. Muundo wa moduli ni kama ifuatavyo:

- Kabla ya kutekeleza moduli ya mafunzo, mwezeshaji awe amepata uelewa wa kutosha wa changamoto na fursa zinazohusiana na upandaji miti na kuongeza thamani katika kijiji.
- Njia ya mafunzo inachukuliwa kulingana na hali halisi, ujuzi na uelewa wa TGA. Hii inamaanisha kuwa mafunzo ya kawaida ya aina kama ya "kitabu cha shule" yana uwezekano wa kutofanya kazi.
- Wanachama wote wa TGA na viongozi wa vijiji wanaalikwa.
- Moduli inajenga uelewa wa Mbinu Zingativu ya Haki za Binadamu, njia shirikishi na jumuishi baina ya uongozi wa TGA na wanachama.
- Wakati wa mafunzo, TGA inapitishwa kwenye mchakato mzima wa upangaji mipango matokeo yake ni mpango kuwa umekamilika (mpango wa mwaka, mpango mkakati au mpango wa biashara)

Katika kuimarisha Kikundi cha wakulima wa miti, uwezo wao wa kupanga mipango na kuitekeleza mipango hiyo itakuwa muhimu kwa uendelevu wao. Kwa sasa, hii ni moja wapo ya sehemu dhaifu za TGA. Inapendekezwa kufanyika kwa uainishaji wa watoa huduma kikamilifu na kwamba mbinu tofauti za uimarishaji uwezo na uaandaaji wa mipango ya TGA zifanyiwe majaribio ndani ya mfumo uliotolewa hapo juu.

## 5.3 Kuimarisha utoaji wa huduma wa TGA

### 5.3.1 Utoaji wa huduma zinazowanufaisha wanachama ni uti wa mgongo wa TGA

Utawala na usimamizi sahihi ndio misingi ya utoaji mzuri wa huduma. Kwa hivyo afua za kuimarisha uwezo zilizoelezewa katika sura iliyopita ni sehemu ya kuimarisha utoaji wa huduma ambazo TGA hutoa kwa wanachama wake. Katiba na mipango ya TGA (mpango kazi, mpango mkakati au mpango wa biashara) inatoa mwongozo wa huduma zipi TGA kiwapatie wanachama wake.

Wanachama wa TGA ni wakulima wa miti. Hivyo, utoaji huduma wa TGA kuwanufaisha wanachama wake inahusiana na kushughulikia mahitaji ya wakulima wa miti katika misitu yao na pia kuwapa fursa mpya za kufaidika na mashamba yao ya miti. Kwa hiyo, kuimarisha utoaji huduma wa TGA ni juu ya kujenga uwezo juu ya maswala ya kiufundi na biashara pamoja na mnyororo wa thamani wa misitu, wakati huo huo kutambua hitaji la kuweza kushughulikia migogoro ya ardhi inayoweza kuwepo na maswala ya haki za binadamu.

Faida kutoka kwa TGA katika namna ya huduma, ni motisha kwa mkulima wa miti kuwa, au kuendelea kuwa, mwanachama wa TGA (na kulipa ada ya uanachama). Malipo kwa ajili ya

huduma ni uti wa mgongo wa uchumi wa TGA imara. Kwa hiyo, kuimarisha utoaji huduma ni suala nyeti kwa TGA kujikimu yenyewe katika kitambo cha muda mrefu. Kuimarisha utoaji huduma kunaweza kumaanisha huduma za ziada (kupanua sanduku la huduma) au upatikanaji, ubora, na gharama za huduma zilizopo.

Kwa afua zilizofadhiliwa (kwa mfano, PFP-2) zinazowalenga wakulima wa miti katika usimamizi wao wa mashamba ya miti (kwa mfano kupunguzia miti) na wakati huo huo kuimarisha TGA kama taasisi, msaada lazima uwe na mambo ambayo wakati huo huo yanaimarisha uwezo wa utoaji wa huduma wa TGA juu ya mada hiyo husika (kwa mfano kupunguzia miti). Kwa hiyo, uwezeshaji wa nje ya darasa unaojikita katika usimamizi wa mashamba ya miti ya wakulima wa miti pekee, hautaimarisha utoaji huduma ya TGA na hatimaye kutoimarisha uendelevu wa shirika.

Ili kuimarisha utoaji wa huduma wa TGA inapendekezwa kuwa dhana ya Wakulima Wakulima wa Miti Mabingwa itambulishwe na kwamba dhana ya Mkulima wa Miti Bingwa ijumuishwe kikamilifu katika taasisi ya TGA. Dira ni kwamba Wakulima wa Miti Mabingwa itakuwa mahali pa kuanzia kwa kuongezeka kwa utoaji wa huduma kupitia TGA na TGA kinavyoendelea kukua watabadilika taratibu na kuwa wataalamu wa misitu wanaopata fursa za ajira kupitia kuajiriwa katika TGA.

### 5.3.2 Wakulima wa Miti Mabingwa

Mkulima wa Miti Bingwa anapaswa kuwa mwanachama wa TGA na awe anaishi ndani ya kijiji husika. Wakulima wa Miti Mabingwa watakuwa ndani ya muundo wa kikundi cha TGA na utoaji wao wa huduma unasimamiwa na uongozi wa TGA. Wakulima wa Miti Mabingwa wanachaguliwa na wanachama wa TGA. Inapendekezwa kwa kuanzia, kuwachagua Wakulima wa Miti Mabingwa wawili katika TGA na kuzingatia usawa wa kijinsia katika uchaguzi. Kipindi cha madaraka cha Mkulima wa Miti Bingwa kinapaswa kufafanuliwa na kila TGA na Mkulima wa Miti Bingwa anaweza kuchaguliwa tena.

Zaidi ya kuwa mwanachama wa TGA na kuishi ndani ya kijiji, inapendekezwa kuwa mahitaji ya Mkulima wa Miti Bingwa yanajumuisha mtu huyo awe anajua kusoma na kuandika, anaheshimiwa na amejidhatiti kupeleka ujuzi wake kwa wakulima wengine wa miti, yaani ajidhatiti katika utoaji huduma.

Wakati wa uwezeshaji wa uteuzi wa Wakulima wa Miti Mabingwa, mkazo unahitaji kuwekwa katika kuthibitisha kiwango cha kujidhatiti baina ya watahiniwa. Wakulima wa Miti Mabingwa watahitaji kuthibitisha wajibu wao wa kuwafikishia ujuzi na maarifa wanachama wengine wa TGA.

Mchakato wa kupatikana Mkulima wa Miti Bingwa katika TGA inapendekezwa kufanyika kama ifuatavyo:

I. Dhana ya Mkulima wa Miti Bingwa inawasilishwa kwa wanachama wa TGA. Uongezaji wa uelewa utajumuisha lengo la kuwa na Mkulima wa Miti Bingwa katika TGA, mahitaji ya Mkulima wa Miti Bingwa pamoja na na taratibu za uteuzi na usimamizi, kuweka wazi jukumu la Mkulima Bingwa ndani ya TGA. Endapo TGA kitaamua kuendelea na kumchagua Mkulima wa Miti Bingwa, mchakato wa uanzishwaji uendelea. Ikiwa sivyo, taratibu za uanzishaji usimame.

II. Wanachama wa TGA wanawabainisha watahiniwa wa Mkulima wa Miti Bingwa na watahiniwa wawasilishwe.

III. Sifa na kujidhatiti kwa watahiniwa kunathibitishwa.

IV. TGA inachagua Mkulima/wakulima wake wa Miti Bingwa.

V. Jina na maelezo ya mawasiliano ya Mkulima wa Miti Bingwa vinarekodiwa kwenye rekodi za TGA na kuzipeleka TTGAU (endapo TGA ni mwanachama wa umoja), pia kwa halmashauri ya wilaya na kwa taasisi inayowezesha (mf. PFP-2).

Wakulima wa Miti Mabingwa watapatiwa mafunzo sawa sawa na wakulima wengine wa miti kwenye ngazi ya kijiji. Kwa nyongeza, Wakulima wa Miti Mabingwa watapata mafunzo zaidi juu ya mada zilizochaguliwa kupitia moduli maalumu za mafunzo zilizotolewa kwa mfano katika

kituo cha FWITC (tazama sura ya 6). Zaidi ya moduli za mafunzo zilizoainishwa katika sura ya 6, inapendekezwa kuwa Wakulima wa Miti Mabingwa pia wapatiwe mafunzo ya ufundishaji, kama vile jinsi ya kutoa huduma za ugani na ushauri na pia kufundisha wengine.

### 5.3.3 Kuimarisha uwezo wa wakulima wa miti katika misitu

Kuimarisha utoaji huduma wa TGA kunahusisha kuongezeka kwa manufaa kwa wanachama kupitia ushauri juu ya maswala ya kiufundi na kibiashara katika mnyororo wa thamani wa misitu. Wakati huo huo kuziinua TGA na kuimarisha uwezo wa wakulima wa miti katika misitu inapendekezwa:

- Afua za kuimarisha uwezo wa wakulima wa miti zinaandaliwa kupitia TGA. Hii inamaanisha kwamba, ingawa namna hii si kuimarisha Kikundi, ila wakulima wa miti wang'amue manufaa wanayopata yanatoka kwenye TGA. Hii hatimaye itakitangaza TGA ndani ya kijiji.
- Dhana ya Mkulima wa Miti Bingwa itambulishwe. Mkulima wa Miti Bingwa ni mkulima wa miti atakayeshiriki katika mafunzo sawa sawa na wakulima wa miti na kwa nyongeza atapatiwa mafunzo zaidi. Mkulima wa Miti Bingwa ataimarisha uwezo wa wakulima wa miti katika misitu kupitia huduma zake, ambazo ni huduma zinazotolewa na yeye mkulima kama sehemu ya shirika la TGA.

Sura ya 6 inaainisha moduli kuu za mafunzo zinazopendekezwa ili kuimarisha uwezo wa wakulima wa miti katika usimamizi wa misitu. Kwa kuongezea juu ya moduli za mafunzo katika ngazi ya kijiji, sura hii inapendekeza moduli maalumu za mafunzo ili kuimarisha utoaji huduma wa TGA kupitia mafunzo kwa Mkulima wa Miti Bingwa au wajasiriamali katika eneo maalumu (mf. FWITC). Kutambua kuwa tathmini ya mahitaji ni msingi wa kujenga uwezo na maeneo yenye kutiliwa uzito kwa ajili ya shughuli za TGA na utoaji huduma kuna uwezekano mkubwa wa kubadilika (mf. matumizi na kuongeza thamani ya mabaki ya miti), inaeleweka kuwa mafunzo yoyote yatahitaji kupangwa kwa undani zaidi na orodha ya moduli za mafunzo iliyopendekezwa hazina mapana sana na zitabadilika kwa kadri muda unavyosonga..

# 6. MODULI ZA MAFUNZO YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MISITU

## 6.1 Utangulizi

Sehemu kuu muhimu ambazo wakulima wa miti wanahitaji huduma na uimarishaji wa uwezo katika misitu yao ni pamoja na:

- Uanzishaji wa kitalu cha miti na usimamizi
- Kuanzishwa kwa shamba
- Usimamizi wa shamba
- Kuzuia na kudhibiti moto
- Upandaji wa miti kama biashara - mambo ya kibiashara ya misitu

Falsafa iliyopo nyuma ya wazo la TGA ni kwamba wakulima wa miti waweze kuwa na kikundi chao kinacho wapatia huduma katika usimamizi wa misitu. Kwa sasa, TGA hazina nguvu za kutosha kushughulikia mahitaji ya wanachama wao. Kwa hiyo, katika uimarishaji wa TGA na wakati huo huo kushughulikia mahitaji ya mkulima wa miti, inapendekezwa kutumia mbinu mbili. Kwanza, afua za kuimarisha uwezo katika za moja kwa moja katika ngazi ya kijiji (kupitia TGA) kwa wakulima wa miti na pili utoaji wa huduma kwa wakulima wa miti kupitia Wakulima wa Miti Mabingwa wa TGA husika.

Linapokuja suala la afua za moja kwa moja za kuimarisha uwezo katika ngazi ya vijiji, inapendekezwa kutumia ushauri wa wafanyikazi na/au watoa huduma pamoja na matukio ya mafunzo yanayohusu sehemu kuu za muhimu zilizoorodheshwa hapo juu. Wakati wa mafunzo katika ngazi ya kijiji wakulima wote wa miti pamoja na Wakulima wa Miti Mabingwa wataalikwa kushiriki.

Kwa kuongezea, inapendekezwa kuwa Wakulima wa Miti Mabingwa wapatiwe mafunzo ya ziada kwenye sehemu maalum (kwa mfano FWITC). Hapa Wakulima wa Miti Mabingwa kutoka TGA kadhaa wanaletwa pamoja ili kupata mafunzo mahususi kwa kina zaidi kwa lengo la kuwajengea uwezo wao wa utoaji huduma.

Mafunzo pendekezwa yamefafanuliwa katika sura ya 6.2 - 6.9. Mafunzo yote yaliyopendekezwa kuanzia ngazi ya kijiji (wakulima wote wa miti) na katika kituo maalumu(Wakulima wa Miti Mabingwa) yanafanunuliwa. Maudhui kwa kila eneo la kupatiwa uzito yanafafanuliwa kwa kifupi (moduli - mada - mada ndogo) pamoja na makadirio yenye mapana ya wakati unaohitajika. Njia ya jumla ni kupunguza muda wa mafunzo katika ngazi ya kijiji kuanzia siku 2 - 3.

Maudhui na muda ulioainishwa katika sura ya 6.2 - 6.9 ni mapendekezo ya jumla. Katika utekelezaji halisi, mafunzo yanapaswa kutegemea tathmini ya mahitaji na mpangilio wa kina juu ya muda na maudhui yaliyo ndani ya muundo wa mpango wa jumla wa mafunzo.

## 6.2 Kuanzisha na kusimamia kitalu cha miti

### 6.2.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji

Kusimamia kitalu na kuuza miche kunatoa fursa nzuri kwa TGA kuwapatia manufaa wanachama wake na kukipatia kipato TGA. Hivyo, kuimarisha uwezo wa usimamizi wa kitalu ni afua muafaka kwa ajili ya yote mawilii kuimarisha utoaji huduma na uendelevu katika TGA.

Lengo la mafunzo ni kwamba TGA kama taasisi au wakulima wa miti mmoja mmoja wawe na ujuzi na maarifa ya kuanzisha na kusimamia vitalu vya miti. Mafunzo yamegawanywa katika moduli 3 na kati ya moduli moja na nyingine malezi na usaidizi wa kivitendo (kwa mfano unaotolewa na maafisa ugani) vinapendekezwa. Mafunzo hayo yanapaswa kuwa ya namna ya kivitendo katika mbinu ya "kujifunza kwa kutenda". Muda wote wa mafunzo ni siku 1 + 3 + 2.

Mafunzo yanahusisha hatua zote katika kusimamia kitalu kutoka kwa uchaguzi wa eneo hadi kuwa na miche iliyo tayari kwa kutolewa. Nyenzo za mafunzo ni pamoja na miongozo[6] na vifaa.

[6] Miongozo ya FDT ya utunzaji wa kitalu inapendekezwa kutumika hapa.

**Jedwali la 3: Mafunzo juu ya uanzishwaji wa kitalu na usimamizi katika ngazi ya vijiji**

| Moduli | Mada | Mada-mahususi | Muda |
|---|---|---|---|
| Maandalizi ya eneo la kitalu cha miti | Kufanya uchaguzi wa eneo la kitalu | Kufanya utafiti wa kiuchunguzi<br>Kusafisha eneo la kitalu cha miti kulingana na ardhi na aina ya udongo | 1 day<br>Siku 1 |
| | Kusanifu na kuandaa eneo la kitalu cha miti | Kuandaa mchoro wa ramani ya eneo la kitalu cha miti<br>Kutoa tafasiri ya mchoro wa ramani<br>Kufanya mpangilio wa kitalu cha miti<br>Kuandaa mchanganyiko wa udongo | |
| Kukuza miche ya miti | Kuzalisha miche ya miti | Kuzalisha miche ya miti kwa kutumia vipandikizi<br>Kufanya ubebeshaji wa miche kwa njia ya vikonyo<br>Kuzalisha miche ya miti kwa njia ya kuotesha vijiti mizizi | Siku 3 |
| | | Andaa sehemu ya kupandia na panda mbegu hapo<br>Kupanda mbegu kwenye sufuria | |
| Kuihudumia miche | | Kupalilia<br>Kuchimba miche<br>Ulinzi dhidi ya wadudu na magonjwa<br>Mbolea | Siku 2 |
| | | Kiwango cha unyevu na kivuli<br>Usumbufu kwenye miche<br>Kupunguzia mizizi<br>Kuhifadhi | |

### 6.2.2 Mafunzo katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa

Jedwali hapa chini linaelezea muhtasari wa mafunzo ambayo FWITC inatumia kujenga uwezo katika uanzishaji na usimamizi wa kitalu. Inapendekezwa kuwa mafunzo haya yanatumika kwa mafunzo ya ndani zaidi ya Wakulima wa Miti Mabingwa. Muda wa mafunzo ni jumla ya wiki 2 (siku 10).

**Jedwali la 4: Mafunzo juu ya uanzishaji wa kitalu na usimamizi katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa [7]**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Kuanzishwa kwa kitalu | Aina za vitalu vya miti | Bainisha aina ya kitalu cha miti (cha muda, cha kudumu, kilicho juu ya ardhi, mizizi wazi, treyi ya kisasa) | Siku 7 |
| | Rekodi za kitalu cha miti | Daftari ya kumbukumbu za kitalu cha miti, uchukuaji wa idadi wa miti kwenye kitalu, ripoti za kitalu cha miti | |
| | Ubunifu wa kitalu cha miti | Uchaguzi wa eneo<br>Kukipangila kitalu<br>Kuanzishwa kwa kitalu | |
| | Maandalizi ya mchanganyiko wa udongo wa kitalu | Mahitaji vya kitalu cha miti<br>Maandalizi ya mchanganyiko wa udongo<br>Uhifadhi wa mchanganyiko wa udongo | |
| | Ukusanyaji wa mbegu za miti | Ubora wa mbegu za miti<br>Zana za kukusanyia mbegu za miti | |
| | Maandalizi ya mbegu za miti | Uchimbaji wa mbegu za miti<br>Ukaushaji wa mbegu za miti na kuzitibu<br>Uwezekano wa kutibu miti na kuhifadhi | |
| | Kupanda mbegu za miti | Matayarisho ya tuta la mbegu<br>Kuandaa viriba na kuvijaza<br>Mbinu tofauti za upandaji<br>Kufanya matibabu kabla ya kupanda mbegu<br>Tumia mbinu tofauti za upandaji mbegu katika kupanda mbegu za miti<br>Kupandikiza miche | |
| | Uhudumiaji miche | Matibabu ya miche na kuilinda<br>Upandaji wa miche na usafirishaji | 3 days<br>Siku 3 |
| | Kutunza kumbukumbu za kitalu cha mbegu za miti | Rejesta ya kitalu cha miti, hesabu ya kitalu cha miti, ripoti za kitalu cha miti | |
| | Usimamizi wa kitalu | Kontena za kienyeji<br>Kitalu cha kisasa (Tray) | |

[7] Training plan as applied in FWITC nursery training

### 6.3 Uanzishwaji wa shamba

#### 6.3.1 Uanzishaji wa mashamba mapya

Mafunzo juu ya uanzishwaji wa mashamba yanatolewa katika ngazi ya kijiji pekee, kwa kuwa hii ni shughuli ya kupata uzoefu kwa vitendo na kuna ufinyu wa manufaa katika mafunzo ya kina katika kituo maalum hasa (kwa mfano FWITC). Lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha kuwa wakulima wa miti wanajua jinsi ya kuanzisha mashamba yao.

Mafunzo yamegawanyika katika moduli mbili: kuandaa ardhi na kupanda. Nyenzo za mafunzo pamoja na miongozo[8] na zana pamoja na vifaa vya kujikinga wakati wa kusafisha ardhi na kupanda. Mafunzo hayo yanapaswa kuelekezwa kwa njia ya "kujifunza kwa kutenda". Muda wote wa mafunzo ni siku 1 + 1.

**Jedwali la 5: Mafunzo juu ya uanzishwaji wa mashamba**

| Moduli | Mada | -Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Maandalizi ya ardhi | Usafi wa ardhi | Kukata na kuondoa miti na vichaka<br>Uchomaji vichaka vilivyokatwa kwa moto uliodhibitiwa<br>Kupalilia | Siku 1 |
| Kuanzishwa kwa shamba | Kupanda miti | Mstari kwa ajili ya mashimo<br>Kuandaa mashimo<br>Kupanda miche<br>Tathmini ya miche iliyoendelea kuwa hai | 1 day<br>Siku 1 |

#### 6.3.2 Usimamizi wa maotea

Usimamizi wa maotea ni mada inayohitajika sana hasa katika wilaya ya Makete, ambapo sehemu kubwa ya misitu ya paina hujiotea kiasilia. Kupitia kilimo bora cha miti, maotea yanabadilika na kuwa misitu mizuri. Kwa kuongezea, kupitia maotea ya miti gharama za awali za utayarishaji wa ardhi na upandaji zinaepukwa na kwa hivyo ni rahisi kuyaendeleza kuliko kupanda. Usimamizi wa maotea ya miti unafanana na ule wa misitu iliyopandwa isipokuwa kwa awamu za mwanzo, ambapo katika maotea ya miti unatakiwa kutengeneza nafasi kati ya mti na mti badala ya kusafisha ardhi na kupanda miti.

Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wanaelewa ni kwanini wafanye kuweka upya nafasi kati ya mti na mti, jinsi ya kuifanya na kwa msongamano wa kiasi gani waiache miti iliyosimama. Mafunzo yanapendekezwa yawe yameandaliwa katika namna ya kivitendo na misitu ya mfano ionyweshe kama mfano.

**Jedwali la 6: Mafunzo juu ya usimamizi maotea**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Uanzishwaji wa shamba la maotea ya miti | Kutengeneza nafasi kati ya mti na mti | Muda kwa ajili ya kuweka nafasi kati ya mti na mti | Siku 1 |
| | | Estimation of target stand density and control of the intensity of respacing<br>Ukadiriaji wa kiasi cha miti kusongamana kinacholengwa na udhibiti wa ugumu wa kuweka nafasi kati ya mti na mti. | |

### 6.4 Usimamizi wa shamba- palizi

Mafunzo juu ya kupalilia yanatolewa katika ngazi ya kijiji tu, kwa kuwa hii ni shughuli ya kivitendo inayofanyika moja kwa moja mahali husika na kuna faida ndogo kama mafunzo ya kina yatafanyika katika kituo maalumu. Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wajue jinsi ya kuteketeza magugu na waelewe umuhimu wa kupalilia wakati wa miaka miwili ya kwanza

[8] Kuna miongozo kadhaa inapatikana mf. kwenye PFP 2 na FDT

baada ya kuanzishwa kwa shamba. Wakati huo huo, inapendekezwa kukuza ufahamu juu ya wadudu na magonjwa ya miti.

Mafunzo yanapendekezwa kuwa ya siku moja, yaliyoandaliwa kwa namna ya "kujifunza kwa kutenda". Ratiba inayopendekezwa wakati wa kupalilia mara ya kwanza na msaada wa ushauri wakati wa kupalilia ni ufuatao:

**Jedwali la 7: Mafunzo ya upaliliaji**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Palizi, wadudu na magonjwa | Kupalilia | Mbinu tofauti za kupalilia: kupalilia kibiashara, kupalilia/ kupalilia mstari, kupalilia kikamilifu, kufyeka | Siku 1 |
| | Udhibiti wa wadudu na magonjwa | Wadudu waharibifu, wadudu warukao, minyoo fundo, magonjwa ya kuvu, magonjwa ya bakteria, magonjwa ya virusi | |

## 6.5 Usimamizi wa mashamba - upogoaji

Mafunzo juu ya upogoaji yanatolewa katika ngazi ya kijiji tu kwani hii ni shughuli inayohusisha utendaji wa kivitendo ya moja kwa moja na kuna faida ndogo ikiwa mafunzo ya kina yatatolewa katika kituo maalumu. Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wanaelewa faida za upogoaji na wanaweza kufanya upogoaji sahihi na salama kwenye mashamba yao.

Mafunzo ni mafunzo ya siku moja na yanapaswa kuwa yameandaliwa kwa namna ya kivitendo kwa mbinu ya "kujifunza kwa kutenda". Inapendekezwa sana kuwa maandalizi yenye umakini yafanyike kabla ya mafunzo. Katika maandalizi, "eneo la mafunzo" (i.e. mashamba ya miti) katika kijiji kilichokubalika na upogoaji ufanyike katika sehemu ndogo ya eneo la mafunzo kabla ya mafunzo, kuonyesha mifano ya upogoaji ulio vizuri. Pia inapendekezwa (endapo ikiwezekana) kuwa mifano iandaliwe katika ratiba zote tatuupogoaji. Misumeno inayofaa kupogolea inapaswa kutambulishwa katika mafunzo. Jambo la kutafakari ni kama misumeno ya kupogoalea inapaswa kutolewa kwa TGA kama boksi la zana ili kukuza utendaji mzuri wa kupogoalea. Zaidi inapendekezwa kuwa Muongozo rahisi wa ukurasa mmoja juu ya upogoleaji uandaliwe na kusambazwa wakati wa mafunzo.

**Jedwali la 8: Mafunzo ya upogoaji**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Upogoaji | Upogoaji | Sababu za upogoaji | Siku 1 |
| | | Ratiba ya upogoaji | |
| | | Mbinu za upogoaji na usalama | |

## 6.6 Usimamizi wa mashamba - kupunguzia miti

***Mafunzo katika ngazi ya kijiji***

Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wanaelewa faida za kufanya upunguziaji wa miti, uchaguzi wa miti na mfululizo wa kupunguzia miti katika mzunguko mzima pamoja na mambo ya kibiashara ya upunguziaji wa miti. Warsha ya mafunzo itajumuisha kuangusha miti, kwani hii ni sehemu inayoambatana ya taratibu za upunguziaji wa miti. Ingawa, matokeo yanayotarajiwa ya mafunzo sio kwamba wakulima wa miti wataweza kwa usalama kutumia msumeno unaofanya kazi kwa nishati ya umeme (chain saw).

**Jedwali la 9: Mafunzo ya kutibu**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Kukonda | Uteuzi wa miti na uvunaji | Faida kutoka kwenye kukonda | Siku 2 |
| | | Uchaguzi wa miti | |
| | | Performing the thinning Kutekeleza kukonda | |
| | Masoko/ uchakataji / matumizi ya miti | Kupanga bei ya miti Kushirikiana na wahusika wa soko Kuongeza thamani | |

Mafunzo hayo ni mafunzo ya siku mbili na yanapaswa kuandaliwa kwa namna ya mbinu ya "kujifunza kwa vitendo". Inapendekezwa sana kuwa maandalizi yenye umakini yafanyike kabla ya mafunzo. Katika maandalizi, "eneo la mafunzo" (i.e. mashamba ya miti) katika kijiji kilichokubaliwa na kupunguzia kunafanyika kwa sehemu ndogo ya eneo la kutolea mafunzo mafunzo kabla ya mafunzo, ili kuonyesha mfano wa kupunguzia kuliko vizuri. Wakati huo huo, miti iliyovunwa itumike kujadili upangaji wa bei na masoko/ matumizi ya miti iliyopunguzwa. Inapendekezwa kuwa Mwongozo rahisi wa ukurasa mmoja juu ya kupunguzia umeandaliwa na kusambazwa wakati wa mafunzo.

Ingawa zinafafanuliwa katika Mwongozo huu kama matukio ya mafunzo yaliyojitenga (kwa sababu kwa sehemu kutokana na malengo tofauti na vikundi tofauti vinavyolengwa, shughuli za uvunaji ni sehemu ya kupunguzia. Kwa hiyo inapendekezwa kwamba warsha za mafunzo kuhusu kupunguzia na uvunaji wa miti ziunganishwe (angalau kwa sehemu) pindi inapowezekana.

### 6.6.1 Mafunzo ya FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa

Huduma inayotarajiwa kwa TGA kutoa kwa wanachama wake inayohusiana na upunguzaji ni pamoja na kuongeza uelewa (yaani kuwashauri wakulima wa miti juu ya hitaji la umbali wa mti na mti), uchaguzi wa mti (kuzuia madalali "kufanya unyonyaji katika bei") na vile vile miunganiko na soko. Kwa hiyo, inapendekezwa kuwa mafunzo yatolewe na FWITC kwa Wakulima wa Miti Mabingwa kuimarisha uwezo wao na hivyo kwa utoaji huduma wa TGA. Mafunzo haya yanapendekezwa kwenda undani zaidi hasa katika uchaguzi wa miti na masuala ya kupanga bei ya miti. Mafunzo yanapendekezwa, hasa linapokuja suala la uchaguzi wa mti, jikite kwenye mafunzo ya vitendo kwenye mashamba ya mfano ya umri tofauti kugusia kwa kadri inavyowezekana mfulizo wa kupunguzia miti katika mzunguko wote.

**Jedwali la 10: Mafunzo uvunaji - kwa wajasiriamali**

| moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Kupunguzia miti | Uchaguzi wa miti na uvunaji | Faida kutokana na upunguziaji | Siku 4 |
| | | Uchaguzi wa miti na mfululizo wa kupunguzia miti katika mzunguko wote | |
| | | Kutekeleza kupunguzia miti | |
| | Masoko/ uchakataji / matumizi ya miti | Upangaji wa bei ya miti<br>Kuwahusisha watendaji katika soko<br>Ongeza thamani | |

## 6.7 Usimamizi wa shamba- uvunaji

Mafunzo haya yanaundwa mahsusi kwa wajasiriamali ambao wanaojihusisha (au watakaohusishwa) katika kuangusha miti na kuvuna baina ya wakulima wadogo wa miti. Lengo la mafunzo ni kuwa na wajasiriamali wenye ujuzi bora katika uvunaji na uchaguzi wa miti (yaani kupunguzia).

**Jedwali la 11: Mafunzo uvunaji - kwa wajasiriamali**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Aina za uvunaji | Kupunguzia | Mfululizo wa kupunguzia miti katika mzunguko wote | Siku 10 |
| | | Uchaguzi wa miti | |
| | Kukata miti | Msitu uliokomaa kukatwa (umri, vipimo, ujazo, n.k) | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutoka kwenye mti hadi gogo | Mbinu za uvunaji | Ukataji miti, ukataji wa matawi, ukataji wa magogo | |
| | Uchumi wa uvunaji | Kuongeza thamani ya mti - mambo ya kiuchumi ya kuzingatia wakati wa kuamua jinsi ya kukata magogo | |
| Matengenezo ya msumeno wa unaotumia nishati | | Kunoa<br>Kusafisha<br>Mafuta na mafuta mazito | |

Kupitia taratibu za ushirikiano mjasiriamali anaweza kuwa mtoa huduma ambaye TGA kinaweza kumtumia na kwa hiyo kuwa sehemu ya utoaji huduma ambayo TGA kinazitoa kwa wanachama wake. Fursa hii inapendekezwa kujadiliwa na TGA ili kujua maslahi yao na vile vile wajasiriamali wenye uwanaowezekano (au walio wajasiriamali tayari) ili kuwahusisha.

Mafunzo ya wajasiriamali inapendekezwa kufanyikia FWITC. Walakini, mafunzo pia yanaweza kuunganishwa (angalau kwa baadhi ya sehemu) na mafunzo juu ya kupunguzia miti kwa wakulima wa miti (sura ya 6.6.1 Kitengo cha mafunzo yanayohama cha PFP-2 kinapendekezwa kutumiwa katika mafunzo ya wajasiriamali. Mafunzo yanapendekezwa yawe ya kujirudia, kwa kutambua kuwa mafunzo ya kujikumbushia yatahitajika mara kwa mara.

## 6.8 Usimamizi wa mashamba - ulinzi na udhibiti wa moto

### 6.8.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji

Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wanaelewa umuhimu wa kuzuia moto, wanajua njia kuu za kuzuia moto na vipengele vikuu vya kupambana na moto wa misitu.

Mafunzo kwa ngazi ya kijiji yanapendekezwa kuwa ya muda wa siku 3. inapendekezwa kuwa eneo la mafunzo liandaliwe kabla ya mafunzo, pamoja na mifano ya njia kuu za kuzuia moto (kupalilia, njia za moto, kizuizi cha moto) pamoja na eneo salama kuonyesha utumiaji wa zana kuu za kuzimia moto (k.m. mapigio ya moto). Mafunzo hayo yanapaswa kuandaliwa kwa namna ya kivitendo yenye mbinu ya "kujifunza kwa kutenda" k.m. kuandaa vizuizi vya moto wakati wa mafunzo na vile vile kutumia vifaa vya kuzimia moto.

**Jedwali la 12: Mafunzo juu ya kuzuia na udhibiti wa moto**

| Moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Kuzuia moto wa misitu | Mbinu za kuzuia | Mbinu upaliliaji | Days<br>Siku 3 |
| | | Njia za moto na vizuizi vya moto | |
| | Usimamizi katika ngazi ya kijiji | Uanzishwaji wa timu ya kudhibiti moto | |
| | | Hatua za uhamasishaji wa umma | |
| Udhibiti wa moto wa misitu | Mbinu za kupambana na moto | Matumizi ya zana tofauti<br>Kushughulikia aina tofauti za moto<br>Hatua za usalama | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Usimamizi katika ngazi ya kijiji | Kuandaa timu za wazima moto | |

### 6.8.2 Mafunzo ndani ya FWITC - kwa ajili ya Wakulima wa Miti Mabingwa

Moto unatengeneza hatari kubwa na changamoto kwenye kilimo cha miti na kuna fursa kwa TGA kutoa uratibu na huduma kutatua haya. Mafunzo katika ngazi ya kijiji (tazama sura iliyopita) hutoa msingi mzuri. Kuimarisha zaidi uwezo wa TGA wa uratibu na utoaji wa huduma inapendekezwa kuwa mafunzo ya ziada yatolewe kwa Wakulima wa Miti Mabingwa na FWITC.

Mafunzo huko FWITC yanapendekezwa kujumuisha mbinu na njia za kuzuia moto, lakini zaidi ya yote zingatia katika mambo ya kujipangilia na kupanga mipango ya kuzuia na kuzima moto. Kwa maneno mengine, vipi usimamizi wa moto unapaswa kupangiliwa na kuratibiwa (timu, majukumu, nk). Kufanya kazi kwa karibu na Halmashauri za Wilaya na TFS ni faida ikizingatiwa kuwa wana uzoefu na wanajihusisha katika mada hii.

Muda unaokadiriwa wa mafunzo ni siku 3 – 5. Mtaala wa mafunzo haya bado haujatengenezwa na inapendekezwa kuwa uandaliwe na PFP-2 kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wakala wa misitu Tanzania (TFS.)

## 6.9 Kulima miti kama biashara - bei ya mbao huundwa[9] vipi

### 6.9.1 Mafunzo katika ngazi ya kijiji

Lengo la mafunzo ni kwamba wakulima wa miti wanaelewa sababu zinazosababisha bei nzuri ya mbao zao. Mafunzo hayo yana pembe kali ya soko la mbao, ukiangalia shamba kutoka kwa mtazamo wa uundaji wa bei.

Mafunzo yanapendekezwa yaandaliwe katika namna ya kivitendo na:

- Mifano ya kivitendo ya mbao zilizochanwa kwa udhibiti wa upotevu wa mbao za ukubwa tofauti tofauti wa magogo. Ikiwezekana, mafunzo yajumuishwe pamoja na matumizi ya kitengo cha mafunzo yanayohama cha PFP-2, vinginevyo kuwe na magogo na vipande vya mbao vilivyochanwa kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa uthabiti.
- Kutembelea mashamba tofauti (yaliyo ndani ya umbali wa kutembea) na kufafanua tofauti ya mvuto wa mashamba hayo kwa wafanyabiashara wa mbao.
- Mifano halisi ya upigaji wa hesabu za bei kwenye karatasi (flip charts) kwa kuanzia na bei ya mbao zilizochanwa katika yadi za mbao zilizo nje ya vijiji.

Muda wa mafunzo unakadiriwa kuwa siku moja. Maandalizi yenye umakini kabla ya mafunzo yanapendekezwa ili kuyafanya mafunzo kuwa na tija kubwa kwa kadri inavyowezekana. Inapendekezwa kuwa kijitabu rahisi cha ukurasa mmoja kiandaliwe na kusambazwa wakati wa mafunzo.

**Jedwali la 13: Mafunzo katika uundaji wa bei ya mbao**

| moduli | Mada | Mada ndogo | Muda |
|---|---|---|---|
| Sababu zinazoamua bei ya mbao | Bei ya mti uliosimama shambani | Uhusiano wa gogo na mbao za m | Siku 1 |
| | | Hali ya mti na ubora wa mti | |
| | Mvuto wa shamba la miti kwa mnunuzi | Mazingira na kufikika kwa shamba | |
| | | Ujazo unaotolewa kuuzwa | |
| | | Market situation<br>Hali ya soko | |

[9] Mafunzo haya yanajikita kwenye upangaji bei wa mbao. Inapendekezwa kwamba mafunzo yanayofanana haya yaandaliwe kwenye “mazao” mengine.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wakulima wa miti fursa za kuchochea bei | Taarifa za bei | Upatikanaji wa habari za bei | |
| | Nguvu ya kushawishi bei | TGA, uimara katika kikundi, ujazo unaouzwa, ujuzi wa bei | |
| | Maamuzi katika usimamizi wa misitu | Msongamano wa miti iliyosimama, upogoaji, kukonda | |

### 6.9.2 Mafunzo katika FWITC - kwa Wakulima wa Miti Mabingwa

Uzoefu kutoka mahali pengine unaonyesha kuwa huduma ambazo wakulima wa miti wamejiandaa kuzilipia ni huduma ambazo zina muunganiko wa moja kwa moja na kipato kutokana na usimamizi wa shamba, m.f. mauzo ya mbao. Kwa hiyo, utoaji wa huduma zenye kuhusiana na uuzaji wa mbao ni fursa kubwa inayowezekana kuchumwa na TGA. Inapendekezwa kuwa mafunzo ya ziada yatolewe na FWITC kwa Wakulima wa Miti Mabingwa kuimarisha uwezo wao na hivyo TGA itoe huduma kwenye masoko ya mbao. Mafunzo haya yanapendekezwa kwenda kwa kina zaidi, kwa muda wa wastani wa siku 3. Mafunzo hayo yanapendekezwa kujumuisha nadharia na mazoezi ya vitendo na yatumie mashine zilizopo FWITC kwa ajili kupata picha ya mambo na pia maeneo ya karibu na ya yadi za mbao zilizopo Mafinga.

# 7. VIAMBATISHO

## Kiambatisho cha 1: Mapendekezo kwa PFP-2

Lengo la PFP-2 ni “kukuza kilimo cha miti endelevu na jumuishi kinachochangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuondoa umasikini”. Linapokuja suala la kuimarisha usimamiaji wa msitu, njia zilizopo ndani PFP-2 za kufikia lengo zinajumuisha kuwafikia wakulima wa miti kwa afua za moja kwa moja kuwaimarisha uwezo na kuimarisha vikundi vya wakulima wa miti.

Ushirika wa wakulima wa miti wenyewe unaotoa msaada kwa wakulima wa miti katika misitu yao ni sehemu kuu ya dira ambayo inaunda msingi wa mbinu ya PFP tangu kuanzishwa kwake mnamo 2010.

Awamu ya pili ya PFP inajikita zaidi katika mbinu wezeshi katika utekelezaji wake, kufanya kazi kwa karibu na mashirika na taasisi. Hii pia iakisiwe katika vile msaada wa kuimarisha mashirika ya wakulima wa miti unatekelezwa.

Inapendekezwa kwamba PFP-2 itazame kwa umakini idadi ya vijiji vya kuvijumuisha katika shabaha yake ili kuwezesha mbinu yenye uzingativu mkubwa na kupata matokeo ya kweli kwenye maeneo husika ya mradi. Chini ni muhtasari wa mapendekezo ya namna kupanga na kutekeleza msaada kwa TGA, yaani kutumia maudhui ya mwongozo huu, ndani ya PFP-2.

**<u>Andaa na tumia ramani ya njia ya uelekeo iliyothabiti kwa ajili uimarishaji wa kishirika</u>**

Hatua katika kuandaa na kutumia “ramani ya njia ya kuiendea” kwa ajili ya uimarishaji TGA zinapendekezwa kuwa kama ifutavyo:

I. Endesha tathimini ya mahitaji ya uwezo katika vijiji vyote vinavyolengwa na PFP-2 kuhusiana na TGA.

   - ✔ Tumia taarifa zilizo kwenye sura ya 3 kuhusu viashiria. Endapo hakuna TGA, ni wazi kwamba uwezeshaji unaanzia kutokea kwenye sifuri.
   - ✔ Tathimini ya mahitaji inapendekezwa kufanyika mara tu vijiji lengwa na PFP-2 vitakapotambulika. Hivyo, tathimini ya mahitaji kuhusu TGA inaweza kutekelezwa punde ndani ya kongani ya Makete na katika kongani nyingine za PFP-2 ifanyike mapema 2021.

II. Andaa mpango wa ujumla wa PFP-2 wa kujenga uwezo wa kitaasisi wa TGA

   - ✔ Mpango wa kujenga uwezo ujumuishe kipindi chote cha PFP-2 na TGA vyote vinavyolengwa. Hii ni dhairi itafanyika kupitia mbinu shirikishi kushirikisha TGA.
   - ✔ Jumuisha ndani ya mpango wa kujenga uwezo maudhui ya ujengaji ya uwezo (m.f.afua za mafunzo) na tumia hatua (sura ya 3) kutambua kwa mapana barabara ya maendeleo katika kila TGA.

III. Uweke mpango wa kujenga uwezo kwenye utekelezaji

   - ✔ Uweke mpango wa kujenga uwezo kwenye utekelezaji katika mpango kazi wa mwaka ukiwa na shabaha mahususi.

Uimarishaji wa kishirika wa TGA usionekane kama mchakato uliojitenga ndani ya PFP-2 bali uunganishwe pamoja na afua nyingine zinazofadhiliwa. Kwa mfano, maendeleo kwa Wajasiriamali (m.f. matumizi ya mabaki ya mbao) yanaweza kufanyika fursa kwa TGA kutoa huduma.

**Kuboresha jukumu la PFP kama mwezeshaji**

Kukuza uendelevu wa hatua za tatuzi za usaidizi ni lazima kuanzishwe ushirikiano wa karibu na mashirika na taasisi zilizopo. Kwa nyongeza,PFP-2 haitakuwa na nguvukazi ya kutekeleza hatua zote za usaidizi. Ni wazi, kuhusisha kokote kwa mtoa huduma kutatakiwa kuzingatia uwezo na rasilimali za mdau anayeshirikishwa.

Mapendekezo ya msingi yanajumuisha:

- Hakikisha utendaji kazi wa mkataba wa mwaka wa utoaji huduma baina ya TTGAU na PFP-2. Utoaji wa ripoti na ufuatiliaji wenye kujikita kwenye utendaji kazi unatoa msingi wa kufikia matokeo katika eneo husika na kutoa uimarishaji wa uwezo kwa TTGAU endapo na pindi inapolazimu. Sawa sawa na maamuzi yaliyochukuliwa na TTGAU, shirika halitajihusisha katika uanzishwaji wa TGA zinazowezeshwa na PFP-2.
- Shirikisha na wahusishe Halmashauri za Wilaya (hasa idara ya misitu na maendeleo ya jamii). Andaa Hati ya Makubaliano kwa ajili ya huduma mahususi na tumia mbinu inayojikita katika utendaji kwenye kuripoti na ufuatiliaji kwa ajili ya matumizi ya rasilimali yenye ufanisi.
- Shirikiana na FWITC na FTI mahususi kwenye mambo yanayohusiana na uimarishaji wa uwezo katika misitu. Tumia mbinu inayojikita katika utendaji katika kuripoti na ufuatiliaji kwa ajili ya matumizi ya rasilimali yenye ufanisi.
- Orodhesha maeneo ya msingi kwa ajili ya hatua za usaidizi, tambua watoa hudama wenye uwezo na andaa Daftari la Mtoa Huduma.
- Kwa kila huduma mahususi ya kutolewa, andaa hadidu za rejea na wafanye watoa huduma mwenye uwezo wafafanuwe jinsi wanavyokusudia kuifikisha huduma. Hii inaunda msingi wa mipangilio ya utoaji huduma inayojikita katika utendaji.

Inapendekezwa kwamba ushirikiano na TTGAU na Halmashauri ya Wilaya ujenge juu ya kilichoainishwa na kukubalika juu ya kushirikishana taarifa, kupanga mipango na njia za kuripoti vile vile juu ya majukumu na wajibu ulioainishwa kinaga ubaga. Kwa mfano, linajapo suala la uimarishaji wa TGA inapendekezwa kuwa Halimashauri za Wilaya na TTGAU zinajihusisha kwa karibu katika mpango kazi wa mwaka wa PFP-2 katika kongani zote ambazo PFP-2 inafanya kazi.

**Kujenga uwezo baina ya wafanya kazi wa PFP-2**

Timu ya PFP-2 ambayo itajihusisha kwa karibu katika uanzishaji na kuimarisha TGA inajumuisha wataalamu, waratibu wa kongani, maafisa ugani na wafanyakazi wa ugani. Uwezo wao wa kuyatekeleza kazi na majukumu yao yahusyo maendeleo ya kishirika ya TGA unahitaji kuthibitishwa na ikilazimika, uimarishwe.

Inapendekezwa kwamba Mtaalamu wa Uchumijamii wa PFP-2 apewe jukumu kama mtu anayetazamwa akibeba jukumu lote kwa ujumla la kusimamia na mwenye wajibu wa hatua saidizi zinazohusu uimarishwaji wa kitaasisi wa TGA.

Inapendekezwa kuwa ujuzi wao na maarifa yao yapimwe na wapatiwe mafunzo kama italazimu katika maeneo yenye umuhimu kama vile:

- Uhusishwaji wa jamii shirikishi, Mbinu Zingativu za Haki za Binadamu na uundaji wa kikundi.
- Uimarishaji wa shirika.
- TGA, ni kitu gani, manufaa yapi ya TGA imara, ni ipi njia ya maendeleo kwa ajili ya TGA na ni zipi changamoto kitakazokabiliana nazo na pia hatua sahihi za kutatua changamoto.

**Kiambatisho cha 2:** Rejea


Agrinatural. 2019. Organizational Strengthening. A Guide to the Coaching Process

FAO. Establishing and Strengthening Farmer Organizations.

Grow Leadership Academy. 2020. RLabs

IFAD. 2013. Strengthening Institutions and Organisations. Synthesis Report.

President's Office, Regional Administration and Local Government Tanzania. 2019. Community Facilitation Manual for Improved Opportunities and Obstacles Development (O&OD)

Project on Private Forestry and Carbon Trading in Tanzania. 2011. Performance Assessment of Service Delivery to Tree Growers' Associations

PFP. 2014. Tree Growing Incentive Scheme Pilot Project

PFP. 2017. Training and Evaluation Report on Fire Prevention and Control to 46 PFP Villages in Iringa, Njombe, Morogoro and Ruvuma Regions.

PFP. 2018. TGA Evaluation Report on Technical and Administrational Capacity to 49 PFP Implementing Villages in Iringa, Njombe, Morogoro and Ruvuma Regions

PFP. 2018. Administration Manual for Tanzanian Tree Growers' Associations

PFP. 2019. Completion Report

PFP. 2020. Human Rights Based Approach and Gender Situational Assessment: A case Study of Makate District. Draft

TTGAU. 2020. Draft TGA Establishment Guideline

**Kiambatisho cha 3: Miongozo na miongozo ya usimamizi wa misitu**

Forestry Development Trust. Moduli Namba 2: Uandaaji sahihi wa kitalu cha miche

Forestry Development Trust. Moduli Namba 3: Uanzishaji wa shamba la miti

Forestry Development Trust. Moduli 4: Usimamizi wa shamba la miti

MNRT, Tanzania. 2017. Forest Plantation and Woodlot Technical Guidelines

MNRT, Tanzania. 2019. Integrated Fire Management, Guidelines for Commercial Forestry.

PFP. 2014. Guidelines for Call for Applications for In-kind Support for Individuals and Organizations – Tree Growing Incentive Scheme

Indufor ...forest intelligence

NIRAS